

**TANROADS**

Serikali imetoa fedha nyingi za kuimarisha miundombinu ya barabara mkoani Ruvuma.

Uk. 7



**TARURA**

Mafanikio makubwa yamepatikana chini ya Rais Samia katika utekelezaji miradi ya barabara Mkoa wa Ruvuma.

Uk.17



**SOUWASA**

Serikali ya Rais Samia imedhamiria kumaliza changamoto ya maji Manispaa ya Songea.

Uk. 21



**MADINI**

Sekta ya madini imepaisha ukuaji uchumi na kuchochea maendeleo mkoni Ruvuma.

Uk. 25

TOLEO MAALUMU MKOA RUVUMA

UHURU ya kijani


ISSN 0876 - 3896 Na. 0010
Alhamisi Aprili 3, 2025 Tanzania

@uhuruonline

MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN

# Ruvuma yajivunia mafanikio makubwa

Rais wa Awamu ya Sita Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. Samia Suluhu Hassan



Pato la Mkoa wa Ruvuma limepanda kutoka shilingi trilioni 5.7 mwaka 2020 hadi trilioni 7.2 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Pato la mtu mmoja nalo limeongezeka kwa asilimia 7.1, likiashiria ustawi wa kiuchumi unaowanufaisha wananchi.



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi Mkoa wa Ruvuma Komredi Odo Mwisho.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo

## MAFANIKIO MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN RUVUMA

# RUVUMA: HATUA KUBWA ZA MAENDELEO CHINI YA UONGOZI WA RAIS SAMIA



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed

Na ALBANO MIDELO

Mkoa wa Ruvuma umeandika historia mpya ya maendeleo katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dk.Samia Suluhu Hassan. Kupitia juhudi za serikali, sekta mbalimbali zimepata msukumo mkubwa, kubadilisha maisha ya wananchi kwa kiwango cha juu.

### UCHUMI WA RUVUMA WAPAA

Pato la Mkoa wa Ruvuma limepanda kutoka shilingi trilioni 5.7 mwaka 2020 hadi trilioni 7.2 mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 20.2. Pato la mtu mmoja nalo limeongezeka kwa asilimia 7.1, likiashiria ustawi wa kiuchumi unaowanufaisha wananchi.

### MAPINDUZI KATIKA SEKTA YA ELIMU

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed anasema katika jitihada za kuinua sekta ya elimu, mkoa wa Ruvuma umefanikiwa kuongeza idadi ya shule za msingi na sekondari, kupanua miundombinu na kuboresha mazingira ya kujifunzia. Miradi kama SEQUIP na BOOST imewezesha ujenzi wa shule mpya, mabweni, vyumba vya madarasa na maabara, hivyo kuleta mwamko mpya wa elimu. Kupitia mradi wa SEQUIP, shule mpya 9 za sekondari zimejengwa kwa gharama ya shilingi 5,044,975,443.00. Mradi wa BOOST umewezesha ujenzi wa shule mpya 12 za msingi pamoja na miundombinu katika shule 44, ukiwa na gharama ya shilingi 7,291,300,000.00.

### HUDUMA ZA AFYA ZABOREKA

Hali ya upatikanaji wa dawa na vifaa tiba imeimarika kutoka asilimia 50 mwaka 2021 hadi



Katibu Tawala wa Mkoa wa Ruvuma Mary Makondo

asilimia 84 mwaka 2024. Zaidi ya vituo 473 vya afya vimeboreshwa, huku hospitali, vituo vya afya na zahanati zikiongezwa na kukarabatiwa kuhakikisha huduma bora kwa wananchi.

### KILIMO NA UCHUMI WA MKOA

Kilimo kimeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Ruvuma. Katika msimu wa 2023/2024, Mkoa umezalisha tani milioni 2.05 za mazao ya chakula, huku mahitaji ya ndani yakiwa tani 470,000 pekee. Hali hii imesababisha ziada kubwa inayouzwa ndani na nje ya nchi, hivyo kuinua kipato cha wakulima.

### UMEME NA MIUNDOMBINU YA MAWASILIANO

Upatikanaji wa umeme umeimarika, ambapo vijiji vyote 554 vya Mkoa wa Ruvuma vimeunganishwa na umeme na kazi ya kupeleka umeme kwenye vitongoji kupitia miradi ya REA inaendelea. Pia uwanja wa ndege wa Songea umeboreshwa ambapo serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 37 kutekeleza mradi huo, Barabara na huduma za mawasiliano zimeboreshwa kwa kiwango kikubwa.

### HATUA KUBWA KWENYE VIWANDA NA BIASHARA

Mkoa wa Ruvuma unaendelea kuwa kitovu cha uwekezaji, ukiwa na viwanda vikubwa sita, viwanda vya kati 25, viwanda vidogo 190 na viwanda vidogo zaidi ya 3,264. Sekta hii imechangia ajira na ukuaji wa uchumi wa ndani.

Kupitia uongozi wa Rais Dk. Samia, Mkoa wa Ruvuma unazidi kung'ara kimaendeleo. Kwa uwekezaji huu mkubwa, ndoto ya Tanzania ya uchumi wa kati wa juu unazidi kukua huku wananchi wakifurahia matunda ya maendeleo endelevu.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, akitunukiwa nishani nne na Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi Tanzania, Jenerali Jacob John Mkunda, kwa niaba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan.



Mkoa wa Ruvuma ni gwiji la chakula nchini ambapo kwa miaka kadhaa sasa mkoa unaoongoza kwa uzalishaji wa vyakula vya nafaka



Mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Ruvuma ukiendelea na ujenzi. Pichani ni jengo la wagonjwa wa nje OPD mradi ambao unatekelezwa katika eneo la Mwengemshndo Manispaa ya Songea

# MAFANIKIO MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN RUVUMA



**Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan akiwa na wanafunzi wa shule ya msingi Chifu Zulu iliyopo Kata ya Mshangano Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma alipofanya ziara ya kikazi na kuifungua shule hiyo iliyojengwa kwa programu ya BOOT**

## MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA: UWEKEZAJI WA KIMKAKATI KATIKA SEKTA YA ELIMU MKOANI RUVUMA

**Na ALBANO MIDELO**

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. Samia Suluhu Hassan, sekta ya elimu mkoani Ruvuma imepata mafanikio makubwa kupitia miradi mbalimbali ya kimkakati.

Afisa Elimu wa Mkoa wa Ruvuma Mwl. Edith Mpinzile anasema uwekezaji huo umeleta maboresho makubwa katika miundombinu ya elimu na kuongeza fursa kwa wanafunzi wengi kupata elimu bora.

**Ongezeko la Taasisi za Elimu**

Mkoa wa Ruvuma umeongeza idadi ya shule kutoka 841 mwaka 2021 hadi 860 ifikapo 2025 kwa shule za msingi, ikiwa ni ongezeko la asilimia 2.3. Kwa shule za sekondari, ongezeko lilikuwa kubwa zaidi, kutoka shule 214 hadi 247, sawa na asilimia 13.3.

Mkoa wa Ruvuma una Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi tisa, Vyuo vya Ufundi Stadi (VETA) vitano, vyuo vya ualimu vitatu na matawi ya vyuo vikuu matatu.



**Muonekano wa shule ya msingi Chifu Zulu iliyojengwa na serikali kupitia Programu ya BOOT katika Kata ya Mshangano Manispaa ya Songea,shule hiyo inachukua wanafunzi wa shule ya msingi na ilizunduliwa Septemba 2024 na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan**

**Fedha na Utekelezaji wa Miradi**

Katika kipindi cha miaka minne (2021/2022 – 2024/2025), mkoa ulipokea jumla ya shilingi bilioni 187.07 kwa ajili ya uboreshaji wa elimu. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 50.15 zilitumika katika mpango wa elimu bila ada, huku bilioni 136.9 zikielekezwa kwenye ujenzi wa miundombinu ya kujifunzia na kufundishia.

Miradi iliyotekelezwa katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan ni pamoja na ujenzi wa madarasa 1,717, maabara 98, shule mpya 53, matundu ya vyoo 3,269, mabweni 102, nyumba za walimu 106, vituo vya walimu 13, ukarabati wa shule kongwe mbili, mifumo ya maji na uzio kwa shule maalumu.

**Uboreshaji wa Shule za Sekondari** Katika ngazi ya sekondari, miradi kadhaa imekamilika ikiwa ni pamoja na ujenzi wa shule mpya 33 za sekondari za kata, ujenzi wa shule moja mpya ya wasichana, ujenzi wa madarasa 1,054, ujenzi wa mabweni 95, matundu ya vyoo 878 na maabara 54.

Mkoa wa Ruvuma pia ulipata magari nane kwa ajili ya shughuli za usimamizi wa elimu na vituo 13 vya walimu viliimarishwa.

Utekelezaji wa miradi ya elimu mkoani Ruvuma umekuwa wa mafanikio makubwa kwa kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Dkt. Samia.

Uboreshaji wa miundombinu na utekelezaji wa sera ya elimu bila malipo umesaidia kuongeza fursa kwa watoto wengi zaidi kupata elimu bora.

Haya ni maendeleo yanayodhihirisha dhamira ya serikali katika kuwekeza kwenye kizazi cha baadaye kwa kuhakikisha mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia.



**Mwonekano wa sekondari ya wasichana ya Mkoa wa Ruvuma ya Dkt.Samia Suluhu Hassan yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,200 wa kidato cha kwanza hadi sita.**

## MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN




**Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan akiweka jiwe la msingi la mradi wa ujenzi wa Bandari ya Mbambabay wilayani Nyasa**





**Mradi wa bandari ya Ndumbi Ziwa Nyasa ambao umetekelezwa na serikali na kukamilika kwa asilimia 100**

# BANDARI ZA NDUMBI NA MBAMBABAY: KUFUNGUA MKOA WA RUVUMA KIMATAIFA

**Na ALBANO MIDELO**

Kasi ya maendeleo katika mwambao wa Ziwa Nyasa, yameendelea kuleta matumaini mapya kwa wakazi wa Wilaya ya Nyasa mkoani Ruvuma.

Serikali ya Awamu ya Sita inayoongozwa na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan imewekeza kiasi kikubwa cha fedha kuboresha miundombinu ya bandari, jitihada ambazo zimefungua fursa nyingi za kiuchumi na usafirishaji katika eneo hilo lenye utajiri mkubwa wa rasilimali.

Ndumbi: Bandari Iliyofufua Uchumi

Kwa miaka mingi, usafiri wa mizigo na abiria katika Wilaya ya Nyasa ulikuwa na changamoto nyingi kutokana na ukosefu wa miundombinu ya kisasa. Hata hivyo, shilingi bilioni 12.2 zilizotengwa kwa ajili ya ujenzi wa bandari mpya ya Ndumbi zimeleta mabadiliko makubwa.

Mbunge wa Jimbo la Nyasa, Mhandisi Stella Manyanya, anasema mradi huo umekamilika kwa asilimia 100 na tayari unatoa huduma kwa ufanisi mkubwa.

Meneja wa Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari za Ziwa Nyasa, Manga Gassaya, anaeleza kuwa bandari ya Ndumbi sasa ina uwezo wa kuhudumia shehena ya mizigo kutoka tani 76,000 hadi tani 110,000 kwa mwaka.

Anasema uwezo wa kuhudumia abiria umeongezeka kutoka 56,000 hadi 126,000 kwa mwaka. "Hii ni hatua kubwa katika kufungua usafirishaji wa ndani na nje ya nchi kupitia Ziwa Nyasa," anasema Gassaya.

Bandari ya Mbambabay: Moyo wa Biashara ya Kimataifa

Mbali na mafanikio ya bandair ya Ndumbi, serikali imetenga shilingi bilioni 81 kwa ajili ya ujenzi wa bandari ya kisasa ya Mbambabay.

Mradi huu unalenga kuimarisha ushoroba wa maendeleo ya Mtwara, ambao ni njia muhimu ya biashara kwa nchi jirani kama Malawi. Kaimu Mhandisi wa Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA), Fabian Paul, anasema ujenzi huo unatarajiwa kukamilika Januari 26, 2026.

Bandari ya Mbambabay itakuwa na gati lenye uwezo wa kuegesha meli mbili zenye uzito wa tani 5,000, jengo la utawala, ghala la kuhifadhi mizigo, nyumba za wafanyakazi na eneo la kuhudumia shehena lenye ukubwa wa mita za mraba 20,000.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, anasisitiza kuwa kukamilika kwa bandari hiyo kutaongeza ukuaji wa uchumi wa Tanzania na kuimarisha mahusiano ya biashara na nchi jirani za Msumbiji na Malawi.

"Hii ni fursa ya ajira kwa vijana wetu na njia bora ya kukuza biashara katika ukanda wa Ziwa Nyasa," anasema Kanali Abbas.

Mustakabali wa Nyasa katika Ramani ya Biashara

Uboreshaji wa bandari hizi mbili si tu kwamba utaimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo, bali pia utachochea uwekezaji wa sekta binafsi katika biashara, kilimo na utalii.

Serikali imeweka mkazo kuhakikisha wananchi wa maeneo haya wananufaika moja kwa moja na maendeleo hayo. "Wananchi washirikishwe kikamilifu ili waone miradi hii ni yao," anasisitiza Kanali Ahmed.

Kwa kasi hii ya maendeleo, Wilaya ya Nyasa inajipanga kuwa kitovu cha usafiri wa majini na biashara ndani na nje ya Tanzania. Hii ni hatua moja kubwa kuelekea maendeleo endelevu ya mkoa wa Ruvuma na taifa kwa ujumla.



**Eneo la bandari ya Mbambabay ambako serikali inatekeleza mradi mkubwa wa ujenzi wa bandari kubwa kuliko zote katika ziwa Nyasa**



**Utekelezaji wa ujenzi wa mradi wa bandari ya Mbambabay ambao umefikia asilimia 22 na mradi unatarajia kukamilika mwaka 2026**



**Muonekano wa bandari ya Mbambabay mradi utakapokamilika kwa asilimia 100**

## MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN



Mashine ya CT Scan ambayo imegharimu zaidi ya shilingi bilioni mbili,imefungwa katika jengo la mionzi katika hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea eneo la Mwengemshindo na tayari imeanza kuwahudumia wananchi



Muonekano wa hospitali ya Halmashauri ya Madaba

# MIAKA MINNE YA RAIS DKT. SAMIA SULUHU HASSAN ILIVYOBORESHA SEKTA YA AFYA RUVUMA

**Na ALBANO MIDELO**

Sekta ya afya nchini Tanzania, hasa katika mkoa wa Ruvuma, imepiga hatua kubwa kufuatia juhudi za serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Dr. Louis Chomboko anasema kupitia uwekezaji wa miundombinu, rasilimali watu na huduma za afya za msingi, maendeleo yamekuwa dhahiri huku wananchi wakishuhudia maboresho makubwa katika upatikanaji wa huduma bora za afya.

**Ongezeko la Vituo vya Afya na Rasilimali Watu**

Mkoa wa Ruvuma una jumla ya vituo 473 vya huduma za afya, ikiwa ni pamoja na hospitali 18, vituo vya afya 50 na zahanati 341.

Hata hivyo, Serikali inamiliki sehemu kubwa ya vituo hivyo ikiwa na hospitali tisa, vituo vya afya 39 na zahanati 277. Pamoja na ongezeko hili, upatikanaji wa watumishi wa afya uko katika asilimia 47.2 huku mahitaji yakiwa watumishi 7,043 dhidi ya waliopo 3,323.

**Maboresho ya Huduma za Afya Kupitia Teknolojia**

Katika kuhakikisha huduma za afya zinaboreshwa, mfumo wa kielektroniki wa serikali (GoTHOMIS) umesimikwa katika vituo 192 kati ya 325, sawa na asilimia 64.74, huku lengo likiwa ni kufikia vituo vyote.

**Upatikanaji wa Dawa na Vifaa Tiba**

Upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeongezeka kutoka asilimia 50 mwaka 2021 hadi asilimia 84 mwaka 2024. Hii ni kutokana na usimamizi thabiti wa serikali, pamoja na ongezeko la ruzuku kwa vituo vya afya.

Kiasi cha shilingi bilioni 7.95 kilitolewa kwa ajili ya dawa na vifaa tiba, huku asilimia 90.1 ya bidhaa zilizohitajika zikifikishwa kwenye vituo vya afya.

**Mafanikio Katika Huduma za Chanjo**

Katika kipindi cha miaka minne, huduma za chanjo zimeimarika, huku baadhi ya chanjo zikifikia viwango vya juu zaidi ya asilimia 100 ya malengo yaliyowekwa. Mfano, chanjo ya kifua kikuu (BCG) imefikia asilimia 166, polio asilimia 135 na HPV asilimia 126.

**Huduma za Uzazi na Mtoto**

Mkoa wa Ruvuma una vituo 348 vinavyotoa huduma za afya ya uzazi na mtoto, ambapo vituo 325 vinatoa huduma ya chanjo na vituo 313 vinatoa huduma ya uzazi na kujifungua.

**Huduma za Saratani ya Mlango wa Kizazi**

Jumla ya wanawake 22,718 walichunguzwa saratani ya mlango wa kizazi, ambapo 301 (asilimia 1.3) waligundulika kuwa na VIA positive na asilimia 87 walitibiwa. Wanawake 79 walihisiwa kuwa na saratani na kupatiwa rufaa kwa uchunguzi zaidi.

**Huduma za Ustawi wa Jamii na Mfuko wa Afya (iCHF)**

Mpango wa usajili wa watoto chini ya miaka mitano umefanikiwa kwa asilimia 119.9, huku watoto 283,094 wakiwa wameandikishwa. Aidha, kaya 31,767 zimejiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa (iCHF), zikichangia shilingi milioni 953 .

**Uwekezaji katika Huduma za Maabara na Uchunguzi wa Magonjwa**

Mkoa umepokea mashine za kisasa za uchunguzi wa magonjwa, ikiwa ni pamoja na mashine 27 za hematolojia, 26 za biochemistry, mashine tisa za Genexpert kwa uchunguzi wa kifua kikuu na mashine nane za X-ray za kidijitali ambazo zimepelekwa kwenye hospitali mbalimbali.

**Maendeleo ya Miundombinu ya Afya**

Serikali imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 4.76 katika miradi 29 ya afya, ambapo miradi 2 imekamilika kwa asilimia 100 na mingine 27 ipo katika hatua mbalimbali za umaliziaji. Kwa mwaka 2024/2025, sh 3.42 bilioni zimetengwa kwa miradi mipya.

Mafanikio haya yanaonesha dhamira ya serikali ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan katika kuboresha sekta ya afya, kwa maendeleo endelevu ya sekta ya afya nchini..



Muonekano wa majengo ya hospitali ya Wilaya ya Tunduru



Muonekano wa majengo ya hospitali ya Wilaya ya Nyasa



Muonekano wa majengo ya hospitali kongwe ya Wilaya ya Tunduru ambayo yamefanyiwa ukarabati na serikali



Mradi wa upanuzi wa hospitali ya Rufaa ya Mkoa,Songea ,jengo la wagonjwa wa nje OPD mradi unaotekelezwa katika eneo la Mwengemshindo Manispaa ya Songea

UHURU ya Kijani

MAONI YA MHARIRI

# Miaka minne ya Rais Dk. Samia ilivyoifungua Ruvuma kiuchumi

SERIKALI ya Awamu ya Sita imeendelea kutekeleza miradi ya maendeleo katika mikoa mbalimbali na lengo ni kuwainua kiuchumi wananchi.

Rais Dk. Samia Suluhu Hassan ameendelea kupeleka fedha nyingi za utekelezaji miradi mijini na vijijini katika mikoa yote nchini.

Miaka minne ya Rais Dk. Samia imekuwa na tija kwa wananchi, ambapo fedha zilizopelekwa katika sekta mbalimbali zimeleta mageuzi makubwa.

Miongoni mwa sekta zilizopata mafanikio makubwa ni pamoja na kilimo, elimu, maji, afya na ujenzi wa barabara.

Mbali na uboreshaji wa sekta hizo, Rais Dk. Samia ametoa fedha nyingi za ujenzi wa miradi mingi ya kimkakati kama ujenzi wa Bwawa la Mwalimu Julius Nyerere, Treni ya Kisasa (SGR) na Daraja la Kigongo-Busisi.

Hivi sasa wananchi wamekuwa wakitumia fursa hiyo kujikwamua kiuchumi kwa kufanya shughuli nyingi za maendeleo kujipatia kipato.

Aidha, Rais Dk. Samia amekuwa akisisitiza dhamira yake ya kuwaletea maendeleo wananchi, ambapo tumeshuhudia wakuu wa mikoa wakitoa maelekezo kwa wataalamu wa miradi wakiwahimiza kuitekeleza kwa wakati na ufanisi.

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa iliyopata mafanikio makubwa katika kipindi cha Serikali ya Awamu ya Sita, ambapo fedha nyingi zimepelekwa kutekeleza miradi mbalimbali.

Fedha hizo zimeboresha sekta ya kilimo, afya, maji, umeme na ujenzi wa miundombinu ya barabara kwa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Katika kipindi cha miaka minne, Ruvuma imeandika historia mpya ya maendeleo chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, ambapo Pato la Mkoa limepanda kutoka sh. trilioni 5.7 mwaka 2020 hadi sh. trilioni 7.2 mwaka 2023. Pato la mtu mmoja limeongezeka asilimia 7.1, likiashiria ustawi wa kiuchumi unaowanufaisha wananchi.

Miradi ya SEQUIP na BOOST imewezesha ujenzi wa shule mpya, mabweni, vyumba vya madarasa na maabara, hivyo kuleta mwamko mpya wa elimu mkoani humo.

Kwa upande wa sekta ya afya, upatikanaji wa dawa na vifaa tiba umeimarika kutoka asilimia 50 mwaka 2021 hadi asilimia 84 mwaka 2024. Pia, zaidi ya vituo 473 vya afya vimeboreshwa.

Vilevile, kilimo kimeendelea kuwa uti wa mgongo wa uchumi wa Ruvuma, msimu wa 2023/2024 ulizalisha tani milioni 2.05 za mazao ya chakula, huku mahitaji ya ndani yakiwa tani 470,000 pekee.

Upatikanaji wa umeme umeimarika, vijiji vyote 554 vya Mkoa wa Ruvuma vimeunganishwa na umeme na kazi ya kupeleka katika vitongoji kupitia miradi ya REA inaendelea.

Chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia, Mkoa wa Ruvuma unazidi kung'ara kwa maendeleo, baada ya kutekeleza kwa vitendo Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) kupitia miradi mingi.

Uchumi wa mkoa huo umeendelea kuwa imara kutokana na kazi nzuri inayofanywa na serikali ya kupeleka fedha nyingi kutekeleza miradi ambayo ni kiungo muhimu cha ukuaji uchumi kwa wananchi wa Ruvuma.

Rai yetu kwa wananchi wa Ruvuma waitumie fursa hiyo, kukuza vipato vyao kupitia sekta mbalimbali kwa sababu tayari serikali imeweka mazingira wezeshi ya upatikanaji mikopo, ikiwemo ya asilimia 10 inayotolewa na halmashauri nchini.

Tunawashauri wananchi wa Ruvuma kuongeza kasi ya kujiletea maendeleo kwa kufanya kazi kwa bidii, juhudi na maarifa kuendelea kukuza pato la mkoa huo.

Mafanikio makubwa yaliyopatikana Ruvuma ni kielelezo cha utendaji makini wa Rais Dk. Samia, ambaye alipoapishwa Machi 19, 2021 aliahidi kuwaletea maendeleo Watanzania, hivyo tunawapongeza viongozi wa mkoa wakiongozwa na Mkuu wa Mkoa Kanali Ahmed Abbas Ahmed.


## Uhuru Publications Limited (UPL)

S.L.P. 9221, Dar es Salaam
Makao Mkuu: Mtaa wa Lumumba Mkabala na Shule ya Msingi Mnazi Mmoja
**Chumba cha Habari:**
+255-739 957 882/FAX: 2183780
email: uhurunews@yahoo.com
uhuruadvert@gmail.com
uhurumakala@gmail.com

**Mkurugenzi Mtendaji Mkuu:** ____________________ 0655 - 355810
**Kaimu Mhariri Mtendaji:** ______________________ 0784 - 333186
**Naibu Mhariri Mtendaji:** ______________________ 0784 - 599717
**Mhariri wa Habari:** ___________________________ 0657 913 894
**Mhariri wa Makala:** ___________________________ 0754 - 305135
**Mhariri wa Michezo:** __________________________ 0652- 161414

IDARA YA BIASHARA
**Meneja Biashara UPL:** _________________________ 0683 - 378522
**Meneja Matangazo:** ___________________________ 0765 - 142207
**Meneja Mauzo na Usambazaji:** __________________ 0715 - 313263

UHURU FM (PMCL)
uhurufmnews@gmail.com
**Kaimu Mkurugenzi Uhuru FM:** _________________ 0765 - 383757
**Kaimu Mhariri Mkuu Uhuru FM:** _______________ 0713 - 248640


# NUKUU



"Katika kuhakikisha barabara zinapitika muda wote, TANROADS mkoa wa Ruvuma imetenga sh. bilioni 17.9 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za muda maalumu na sehemu korofi.

**MHANDISI Salehe Juma**



"Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeonyesha dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Songea kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo.

**WAKILI Bashiri Muhoja**



"Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inaleta matokeo chanya na kuchangia katika maendeleo ya taifa kwa ujumla.

**AMINA Khamis Sefu**



"Tunachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio haya makubwa katika sekta ya miundombinu. Kupitia ongezeko la fedha kupitia Mfuko wa Majimbo na Tozo za mafuta, wananchi wa Ruvuma wamefaidika na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, jambo ambalo limewezesha usafiri wa haraka na rahisi wa mazao na huduma nyingine.

**MHANDISI Silivester Chinengo**



"Utafiti uliofanywa Mwaka 2001, kwenye mgodi wa Ngaka wilayani Mbinga, ulibaini kuwepo kwa madini ya makaa ya mawe yanayoongoza kwa ubora duniani kiasi cha tani milioni 400.

**BOSCO Mabena**

## ENZI HIZO



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma, Anne Makinda, akinyanyua ngao baada ya kukabidhiwa na Rais Benjamin Mkapa, ikiwa ni zawadi ya mkoa huo katika sherehe za uzinduzi wa Mbio za Mwenge wa Uhuru. Hiyo ilikuwa mwaka 1997.

# WAKALA YA BARABARA TANZANIA TANROADS
OFISI YA MENEJA MKOA WA RUVUMA




**Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan akifungua barabara ya lami kutoka Mbinga hadi Mbambabay yenye urefu wa kilometa 66,hafla ya uzunduzi huo ilifanyika mjini Mbambabay wilayani Nyasa.**

# MAFANIKIO TANROADS

TANROADS Mkoa wa Ruvuma inasimamia mtandao wa barabara wa kilometa 2,166.20, zikiwemo barabara kuu na barabara za mkoa.

## SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA BARABARA RUVUMA

**MIRADI MIKUBWA YA MAENDELEO**

**UJENZI WA BARABARA YA MBINGA – MBAMBA BAY**

Barabara ya kilometa 66 ilijengwa na kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kwa gharama ya Tsh. 129.36 bilioni. Mradi huu ulizinduliwa tarehe 24 Septemba 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan.







**Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Salehe Juma**

MAFANIKIO TANROADS




**Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan akikata utepe kuifungua rasmi barabara ya Mbinga-Mbambabay ambayo serikali ilitoa zaidi ya shilingi bilioni 129 kuijenga yenye urefu wa kilometa 66.**

# SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA BARABARA RUVUMA

**Na ALBANO MIDELO**

Serikali kupitia Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) inaendelea na juhudi za kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja mkoani Ruvuma.

Lengo kuu ni kurahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa, hivyo kuchochea uchumi na kupunguza umaskini.

TANROADS Mkoa wa Ruvuma inasimamia mtandao wa barabara wa kilometa 2,166.20, zikiwemo barabara kuu na barabara za mkoa.

**BAJETI NA UTEKELEZAJI WA MIRADI**

Meneja wa TANROADS Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Salehe Juma anasema katika kutekeleza majukumu yake, TANROADS inasimamia miradi mikubwa ya maendeleo, miradi midogo ya maendeleo, pamoja na matengenezo ya barabara na madaraja.

Miradi hiyo inatekelezwa kwa bajeti inayosimamiwa kupitia Makao Makuu ya TANROADS kwa kushirikiana na serikali na wadau wa maendeleo.

**MIRADI MIKUBWA YA MAENDELEO**

**UJENZI WA BARABARA YA MBINGA – MBAMBA BAY**

Barabara hiyo ya kilometa 66 ilijengwa na kampuni ya China Henan International Cooperation Group Co. Ltd (CHICO) kwa gharama ya sh. bilioni 129.36. Mradi huu ulizinduliwa Septemba 24, 2024 na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dk. Samia Suluhu Hassan.

**UJENZI WA DARAJA LA RUHUHU**

Daraja lenye urefu wa kilometa 98.01 linaunganisha Wilaya ya Nyasa (Ruvuma) na Ludewa (Njombe). Ujenzi wake ulikamilika Oktoba 15, 2021 kwa gharama ya sh. bilioni 8.976.

**UKARABATI WA UWANJA WA NDEGE SONGEA**

Ukarabati wa uwanja huo ulianza Aprili 2019 na kukamilika Machi 2023 kwa gharama ya sh.bilioni 37.09. Mradi huo ulikuwa kwenye kipindi cha uangalizi hadi Septemba 2024.

**UJENZI WA BARABARA YA KITAI - LITUHI - NDUMBI**

Mradi huu wa kilomita 95.3

**KILOMITA 2,166.20**

**Kiwango cha mtandao wa barabara unaosimamiwa na TANROADS Mkoa wa Ruvuma zikiwemo barabara kuu na barabara za mkoa.**

MAFANIKIO TANROADS

# SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA BARABARA RUVUMA

unatekelezwa kwa awamu tatu kwa kiwango cha lami:

- Kitai – Amani Makoro (Km 5): Ulianza Juni 2019 na kukamilika Agosti 2020 kwa sh. bilioni 6.957.
- Amani Makoro – Ruanda (Km 35): Ujenzi ulianza Juni 2022 na unatarajiwa kukamilika Aprili 2024 kwa sh.bilioni 60.481.
- Ruanda – Lituhi – Ndumbi (Km 50): Ujenzi unaendelea kwa sh. bilioni 95.76 na unatarajiwa kukamilika Juni 2026.

**UJENZI WA BARABARA YA LIKUYUFUSI – MKENDA**

Barabara hii ya kilometa 124 ipo kwenye hatua za mwisho za kusainiwa kwa mkataba wa ujenzi. Fidia ya sh. bilioni 5.19 imeshatathminiwa na kusubiri malipo kutoka Wizara ya Fedha.

**UJENZI WA BARABARA YA LUMECHA - LONDO–MALINYI - LUPIRO**

Barabara hiiyo ya kilometa 512 inaunganisha mikoa ya Ruvuma na Morogoro. Serikali imesaini mkataba na kampuni ya China Civil



Mradi wa ujenzi wa barabara ya kutoka Mbinga hadi Mbambabay wilayani Nyasa iliyogharimu zaidi ya shilingi bilioni 129

MAFANIKIO TANROADS

# SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA BARABARA RUVUMA




Ukarabati na upanuzi wa uwanja wa Ndege wa Songea ambao serikali imetoa zaidi ya shilingi bilioni 37 kutekeleza na kuongeza idadi ya abiria wanaotumia uwanja huo



Mradi wa daraja la Mkenda lilaounganisha Tanzania na Msumbiji kupitia wilaya ya Songea,daraja hilo linatarajiwa kupanuliwa.



Mradi wa daraja la Ruhuhu linalounganisha Mkoa wa Ruvuma na Njombe

Engineering Construction Corporation Ltd (CCECC) kwa ajili ya utekelezaji wa mradi huo kwa sasa utatekelezwa kwa mfumo wa sanifu na jenga (design and build) ndani ya miezi 66.

**UJENZI WA BARABARA YA SONGEA – LUTUKIRA NA MCHEPUKO WA SONGEA**

Mradi huo wa kilomita 116 unafadhiliwa na Benki ya Dunia. Ujenzi unatarajiwa kuanza wakati wowote baada ya kukamilika kwa mchakato wa zabuni.

**MIRADI YA MADARAJA**

**DARAJA LA MITOMONI**

Daraja lenye urefu wa mita 45 linaunganisha Wilaya za Nyasa na Songea Vijijini. Mradi huo utatekelezwa kwa miezi 15 kwa gharama ya sh. bilioni 9.29 kwa ufadhili wa Serikali na Benki ya Dunia.

**DARAJA LA MKILI**

Daraja la Mkili lina urefu wa mita 20 na linajengwa kwa sh. bilioni 3.19 kwa muda wa miezi 15.

**DARAJA LA MKENDA**

Mchakato wake ulisitishwa kutokana na kujitokeza kwa mkandarasi mmoja




Taa za barabarani katika eneo la Mbambabay wilayani Nyasa mkoani Ruvuma.

MAFANIKIO TANROADS



# SERIKALI YAENDELEA KUIMARISHA MIUNDOMBINU YA BARABARA RUVUMA



Mradi wa daraja la Ruhuhu linalounganisha Mkoa wa Ruvuma na Njombe

aliyekuwa amewasilisha gharama za juu kuliko makisio ya wakala.

**USANIFU WA BARABARA**

Mbali na miradi inayoendelea, TANROADS inaendelea na usanifu wa barabara na madaraja muhimu kama:

• Barabara ya Mbamba Bay – Lituhi (Km 112.4)
• Barabara ya Mtwarapachani – Nalasi – Tunduru (Km 300)
• Barabara ya Madaba – Mundindi – Liganga – Mkiu (Km 46)

**MATENGENEZO YA BARABARA NA HIFADHI YA BARABARA**

Katika kuhakikisha barabara zinapitika muda wote, TANROADS mkoa wa Ruvuma imetenga sh. bilioni 17.9 kwa ajili ya matengenezo ya barabara za muda maalumu na sehemu korofi.

Aidha, jitihada za kuhifadhi hifadhi ya barabara zinaendelea kwa kuweka vigingi na kutoa notisi kwa wavamizi.

Juhudi za serikali kupitia TANROADS mkoa wa Ruvuma zinaendelea kuleta maendeleo kwa kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja.

Haya yote yanalenga kuinua uchumi wa wananchi kwa kurahisisha usafiri, kuunganisha mikoa na kuimarisha sekta ya uchukuzi nchini.

## MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN

# RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA SEKTA YA UTALII MKOANI RUVUMA



Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan alipotembelea Makumbusho ya Taifa ya Majimaji mjini Songea

**Na ALBANO MIDELO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt Samia Suluhu mtalii namba moja nchini, amedhamiria kuboresha sekta ya utalii na kuhamasisha Watanzania kufanya utalii wa ndani kuongeza mapato.

Pia ametoa mabilioni ya fedha katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere kujenga lango la Namtumbo mkoani Ruvuma na ametoa fedha kuboresha bustani ya Ruhila Manispaa ya Songea kuhakikisha sekta ya utalii inafunguka mkoani Ruvuma.

Akiwa ziarani mkoani Ruvuma Septemba 2024 alitembelea baadhi ya vivutio vya utalii ikiwemo makumbusho ya Taifa ya Majimaji yaliyopo mjini Songea na kanisa kongwe lililosheheni historia la Peramiho nje kidogo ya Mji wa Songea.

Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa mikoa michache nchini ambayo imebarikiwa na Mwenyezi Mungu kuwa na vivutio vya aina zote za utalii, ambazo ni utalii wa ikolojia na utamaduni.

**VIVUTIO VYA UTALII WILAYA YA SONGEA**

MJI wa Songea ni miongoni mwa maeneo machache nchini ambayo yana hazina kubwa ya utajiri wa kihistoria na kishujaa.

Mji wa Songea ulianzishwa mwaka 1897 kama kituo cha kijeshi cha Kijerumani. Historia inaonesha kuwa Mji wa Songea uliathirika na Vita ya Majimaji kati ya mwaka 1905 hadi 1907.

Licha ya Mji huo kuathirika na vita hivyo, uliendelea kuwa Makao makuu ya Mkoa wa Ruvuma wakati wa utawala wa Waingereza katika Tanganyika, baada ya uhuru hadi leo bado Songea ndiyo Makao Makuu ya Mkoa wa Ruvuma.

Mji wa Songea una umaarufu wa mashujaa wa Vita ya Majimaji ambapo mashujaa 67 walinyongwa mwaka 1906 kati yao mashujaa 66 walizikwa katika kaburi moja.

Nduna Songea Mbano ambaye alikuwa na umaarufu, alinyongwa na kuzikwa katika kaburi lake ambapo makaburi yote yapo katika Makumbusho ya Taifa ya Majimaji Songea.

> **1897**
>
> **Mwaka ambao mji wa Songea ulianzishwa kama kituo cha kijeshi cha Kijerumani. Historia inaonesha kuwa Mji wa Songea uliathirika na Vita ya Majimaji kati ya mwaka 1905 hadi 1907.**

Haya ni Makumbusho pekee nchini ambayo yamebahatika kuwa na vifaa muhimu katika historia ya Mtanzania. Mji wa Songea ni miongoni mwa miji michache ambayo ilitoa upinzani mkali katika vita ya Majimaji.

Katika Makumbusho hayo kuna ushahidi ambao unaonesha moja kwa moja kuwa wazee wa Songea walishiriki kikamilifu katika vita hiyo.

**MTO RUVUMA ULIVYOUBEBA MKOA WA RUVUMA**

Mto Ruvuma wenye urefu wa kilometa 800 ni miongoni mwa vivutio vya utalii vya kipekee mkoani Ruvuma. Mto huo ndiyo Mto mrefu kuliko yote katika nchi za Afrika Mashariki na kati na miongoni mwa mito maarufu barani Afrika ukiwa umeanzia kwenye misitu ya milima ya Matogoro Manispaa ya Songea na kumwaga maji yake Bahari ya Hindi.

Mto Ruvuma unapita katika wilaya zote tano za mkoa wa Ruvuma ambazo ni Songea, Nyasa, Mbinga, Namtumbo na Tunduru unaendelea na safari yake hadi katika daraja la umoja wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara na kuendelea hadi mkoani Mtwara na kumwaga maji yake katika Bahari ya Hindi.

**PERAMIHO ILIVYOSHEHENI VIVUTIO VYA KIHISTORIA**

**Mji** wa Peramiho uliopo Wilaya ya Songea Mkoa wa Ruvuma ni miongoni mwa miji ya zamani yenye historia ya kipekee katika ukanda wa kusini.

Mji huo unafahamika zaidi nje ya nchi pengine kuliko miji mingine iliyopo kusini mwa Tanzania kutokana na mji huo kuwa na historia ya kipekee ikiunganisha Tanzania na mataifa ya Ulaya.

Wabeneditine hao waliingia kwa mara ya kwanza katika mji huo mkongwe mwaka 1898 wakiongozwa na Kasian Spiss. Tangu wakati huo Wabenediktine









Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan alipotembelea Kanisa kongwe lililosheheni utajiri wa historia la Peramiho wilayani Songea mkoani Ruvuma

## MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA SULUHU HASSAN





**Hifadhi ya msitu wa mazingira asilia ya Mwambesi wilayani Tunduru ambayo pia imepitiwa na Mto Ruvuma ambako sasa unafanyika utalii wa kupiga kasia kwa kutumia mitumbwi**

# RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA SEKTA YA UTALII MKOANI RUVUMA

hao wamekuwa wakifanya mambo yanayoutangaza mji huo hali iliyosababisha kuutambua mji wa Peramiho kuwa ni mji unaokidhi vigezo kuwa mji wenye utalii wa kiutamaduni.

**VIVUTIO VYA UTALII WILAYA YA NYASA**

Wilaya ya Nyasa ambayo makao makuu yake ni Mbambabay una fursa za maliasili ya kutosha zikiwemo Ziwa Nyasa, visiwa, wanyamapori, samaki, mito, fukwe, mawe ya ajabu, milima ya Livingstone na mali kale ambazo hazijaharibiwa, hivyo kuifanya wilaya ya Nyasa kuwa benki ya vivutio vya utalii na uwekezaji.

**VIVUTIO VYA UTALII TUNDURU**

Wilaya ya Tunduru imebarikiwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali ukiwemo msitu wa Hifadhi wa Taifa wa mazingira asilia Mwambesi ulianzishwa mwaka 1956.

Msitu huo umepandishwa hadhi kuongeza uhifadhi zaidi kutokana na kuwa na utajiri wa viumbe vya kipekee duniani wakiwemo wanyama, ndege na mimea.

Katika msitu wa Mwambesi kuna jamii ya ndege maarufu duniani anayeitwa Pentiole ambaye utafiti umebaini kuwa ndege huyo amehamia kutoka Madagaska baada ya mazingira aliyokuwa anaishi kuharibiwa na shughuli za kibinadamu.

Ndege huyu wa aina yake ni miongoni mwa vivutio adimu katika hifadhi ya msitu asilia wa Mwambesi ambao unavutia watalii wengi wa ndani na nje ya nchi.

> Jiwe la Mbuji limekuwa gumzo kwa wengi waliosikia taarifa za kivutio

**VIVUTIO VYA UTALII NAMTUMBO**

Wilaya ya Namtumbo imebarikiwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali ikiwemo kupitiwa na Hifadhi ya Taifa ya Nyerere inayounganisha Mikoa minne ya Ruvuma, Pwani, Lindi na Morogoro.


Katika Mkoa wa Ruvuma hifadhi hii inapatikana katika wilaya za Namtumbo na Tunduru. Tunamshukuru na kumpongeza Mhe. Rais kwa kuendeleza hifadhi ya Nyerere ndani ya Mkoa wa Ruvuma, ambayo inakwenda kuchochea ukuaji wa uchumi ndani ya mkoa na Taifa kwa ujumla.

Moja ya jamii ya miti ambayo haijafahamika na kutangazwa ipasavyo iliyopo katika hifadhi ya Taifa ya Nyerere ni magogo ya miti iliyogeuka mawe ambayo kitaalam inaitwa ***fossilized tree trucks***. Magogo hayo yanapatikana katika msitu wa Mbati wilayani Tunduru.

**VIVUTIO VYA UTALII WILAYA YA MBINGA**

Wilaya ya Mbinga imebarikiwa kuwa na vivutio vya aina mbalimbali ikiwemo Jiwe la Mbuji ambalo lipo katika wilaya ya Mbinga ni miongoni mwa vivutio adimu na vya kipekee, jiwe la Mbuji.

Jiwe la Mbuji limekuwa gumzo kwa wengi waliosikia taarifa za kivutio hicho. Neno Mbuji kwa lugha ya kabila la Wamatengo ni **"Kitu kikubwa"**, jiwe hilio lipo katika kijiji cha Mbuji kata ya Mbujii na limekuwa kivutio adimu kwa wageni wa ndani na nje ya nchi.



**Eneo la ziwa Nyasa katika mji wa Mbambabay amnbalo unafanyika uwekezaji mkubwa baada ya Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan kutoa zaidi ya shilingi bilioni 81 kujenga Bandari ya kisasa inayotarajiwa kukamilika Januari 2026**



**Kisiwa cha Lundo ziwa Nyasa ambacho kinamilikiwa na TAWA ambao wameweka wanyamapori katika ,kisiwa hicho hivyo kuvutia watalii**



**FUKWE za kuvutia Ziwa Nyasa wilayani Nyasa mkoani Ruvuma zinazofaa kwa uwekezaji**





**Chanzo cha mto Ruvuma unaoanzia milima ya Matogoro mjini Songea na mwonekano wa Mto Ruvuma eneo la Namtumbo.**




# TANESCO

## MIAKA MINNE YA MAFANIKIO





Vifaa na eneo la ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme Gridi ya Taifa wilayani Tunduru mkoani Ruvuma.

> **"Kwa sasa, tunashuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wetu hasa katika maeneo ya vijijini ambako umeme unachochea maendeleo ya biashara ndogo ndogo, viwanda vidogo, na huduma za kijamii afya na elimu.**

# Nishati ya umeme yazidi kuangazia maisha ya wananchi wa Ruvuma

**WASILIANA NASI RUVUMA**
**Anuani ya Posta: P.O.BOX 5, Songea Simu: +255 025 2602048 Simu ya Mkononi: +255 737 683544 Barua Pepe: songearrh@afya.go.tz**

MAFANIKIO TANESCO

# Nishati ya umeme yazidi kuangazia maisha ya wananchi wa Ruvuma



NAIBU Waziri wa Nishati, Mhe. Judith Kapinga akikata utepe kabla ya kubonyeza 'switch' kuwasha taa, kuashiria umeme umefika kwa mara ya kwanza katika Kijiji cha Litumbandyosi Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma, kushoto kwake mwenye shati la kijivu ni Mbunge wa Jimbo la Mbinga Vijijini, Mhe. Benaya Kapinga, Tarehe 8 Oktoba, 2023.

**Na ALBANO MIDELO**

Katika pembe za kusini mwa Tanzania, maendeleo ya miundombinu ya umeme yameendelea kufungua fursa mpya kwa wakazi wa mkoa wa Ruvuma.

Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), kwa kushirikiana na Wakala wa Nishati Vijijini (REA), limefanikiwa kutekeleza miradi mikubwa ya usambazaji wa umeme, hatua inayobadilisha maisha ya maelfu ya wananchi.

**Hatua Kubwa Katika Usambazaji wa Umeme**

Mkoa wa Ruvuma unajumuisha wilaya tano ambazo ni Songea, Mbinga, Nyasa, Namtumbo, na Tunduru.

Kulingana na ripoti ya TANESCO, vijiji vyote 554 vya mkoa wa Ruvuma vimeunganishwa na umeme, huku vitongoji 2,056 kati ya 3,762 vikiwa tayari na huduma hiyo. Hii ni hatua kubwa inayochochea maendeleo ya uchumi, biashara, na ustawi wa jamii.

Meneja wa TANESCO Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Eusebius Mhelela,anabainisha kuwa miradi ya usambazaji wa umeme imeimarika kwa kasi kutokana na uwekezaji wa zaidi ya shilingi bilioni 146.

"Kwa sasa, tunashuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wetu, hasa katika maeneo ya vijijini ambako umeme unachochea maendeleo ya biashara ndogondogo, viwanda vidogo, na huduma za kijamii kama afya na elimu," anasema Mhandisi Mhelela.

> **"Kwa sasa, tunashuhudia mageuzi makubwa ya kiuchumi kwa wananchi wetu, hasa katika maeneo ya vijijini ambako umeme unachochea maendeleo ya biashara ndogondogo, viwanda vidogo, na huduma za kijamii kama afya na elimu.**
>
> **Meneja wa TANESCO Mkoa wa Ruvuma, Mhandisi Eusebius Mhelela**

**Miradi Mikubwa ya Nishati Inayoendelea**

Miradi mikubwa inayotekelezwa kwa sasa inajumuisha REA Awamu ya Tatu, Mzunguko wa Pili, inayogharimu shilingi bilioni 91.5, Mradi wa Ujazilizi (Densification 2C) wenye thamani ya shilingi bilioni 33, na Mradi wa Kupeleka Umeme kwenye Migodi, Kilimo, na Biashara wa shilingi bilioni 5.5.

Hii ni dalili tosha kwamba serikali inaendelea kuwekeza kwa nguvu katika nishati kwa ajili ya maendeleo ya wananchi wake.

Katika Jimbo la Peramiho, kwa mfano, zaidi ya asilimia 99 ya mradi wa REA III Round II umekamilika, ambapo vijiji 28 vimepata huduma ya umeme. Hali kama hiyo inajitokeza katika maeneo mengine kama Mbinga, Nyasa, na Namtumbo, ambako wakazi wanaendelea kufurahia huduma bora ya umeme.

**Faida kwa Wananchi**

Moja ya mafanikio makubwa yanayoletwa na miradi hii ni kuimarika kwa huduma za afya, elimu, na biashara. Vituo vya afya vimeunganishwa na umeme, kurahisisha uhifadhi wa dawa na uendeshaji wa vifaa vya matibabu kama mashine za X-ray.

Baadhi ya Shule mkoani Ruvuma zimeanza kutumia teknolojia ya kisasa katika ufundishaji, huku wakulima wakinufaika na matumizi ya mashine za kusindika mazao.

"Awali, tulikuwa tukilazimika kusaga unga kwa kutumia mikono, lakini sasa tuna mashine zinazotumia umeme, jambo ambalo limeongeza uzalishaji na kuokoa muda," anasema Bi. Anna Mwenda, mfanyabiashara wa Mbinga.

Katika hatua nyingine ya maendeleo,TANESCO imeanzisha kampeni ya uhamasishaji kwa wananchi ili kuwalinda miundombinu ya umeme. Pia, serikali imeanza mradi wa ujenzi wa njia ya msongo wa kilovolti 220 kutoka Songea hadi Tunduru, mradi unaogharimu shilingi bilioni 150.78.

**Hatma ya Nishati Mkoani Ruvuma**

Kwa ujumla, mkoa wa Ruvuma unashuhudia mageuzi makubwa kupitia uwekezaji wa umeme. Kuimarika kwa huduma hii kunatarajiwa kuongeza uzalishaji wa viwanda, kukuza sekta ya kilimo, na kuboresha maisha ya wananchi kwa ujumla.



VIFAA na eneo la ujenzi wa mradi mkubwa wa umeme Gridi ya Taifa Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma.

*Mradi unafadhiliwa na serikali kuu wa njia ya msongo wa 220kV kutoka Songea hadii Tunduru, ikiwa na lengo la kuboresha upatikanaji wa umeme na kujenga vituo vya kupoza umeme . Katika Mkoa wa Ruvuma mradi unatekelezwa na Mkandarasi Kalpataru Projects International Limited kutoka India.*

*Gharama za mradi huu ni Shilingi za Kitanzania bilioni 150.78. Mradi huu una urefu wa kilomita 214.5. Mradi unahusisha pia ujenzi wa kituo cha kupoza umeme katika Wilaya ya Tunduru chenye ukubwa wa 2x60MVA cha msongo wa kilovolti 220/33. Muda wa utekelezaji wa mradi ni miezi 18,*

# MAFANIKIO YA MAMLAKA YA MAPATO TANZANIA MKOA WA RUVUMA CHINI YA UONGOZI WA RAIS SAMIA




**Kamishna Mkuu wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) Yusuph Mwenda akimkabidhi tuzo Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed kwa walipakodi bora wa Mkoa wa Ruvuma zilizotolewa na TRA.**

**Na ALBANO MIDELO**

MAMLAKA ya Mapato Tanzania (TRA) Mkoa wa Ruvuma inasimamia ukusanyaji wa kodi katika wilaya tano za mkoa huu Songea, Mbinga, Tunduru, Namtumbo na Nyasa.

Kituo cha huduma kwa mlipakodi kipo katika Halmashauri ya Wilaya ya Madaba, pamoja na vituo vya forodha katika Mkenda Nakawale na Mbambabay.

**Makusanyo ya Mapato kwa Kipindi cha Julai 2023 - Juni 2024**

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Juni 2024, TRA Mkoa wa Ruvuma ilipangiwa lengo la kukusanya shilingi 17,430,066,646.00 na kufanikisha kukusanya shilingi 20,328,874,383.54, ikiwa ni asilimia 117 ya lengo.

Makusanyo ya kila mwezi yalikuwa kama ifuatavyo:

- Julai 2023: 1,079,308,537.07 (asilimia 82 ya lengo)
- Agosti 2023: 1,507,280,993.95 (asilimia 119 ya lengo)
- Septemba 2023: 2,335,012,733.36 (asilimia 159 ya lengo)
- Oktoba 2023: 1,645,259,340.66 (asilimia 120 ya lengo)
- Novemba 2023: 1,540,433,795.22 (asilimia 117 ya lengo)
- Desemba 2023: 2,268,030,249.85 (asilimia 120 ya lengo)
- Januari 2024: 1,432,462,570.13 (asilimia 106 ya lengo)
- Februari 2024: 1,501,852,020.67 (asilimia 115 ya lengo)
- Machi 2024: 1,831,412,515.50 (asilimia 118 ya lengo)
- Aprili 2024: 1,571,505,892.51 (asilimia 119 ya lengo)
- Mei 2024: 1,351,391,101.54 (asilimia 100.4 ya lengo)
- Juni 2024: 2,328,874,383.54 (asilimia 121 ya lengo)

Jumla ya makusanyo kwa kipindi hicho ni shilingi 20,392,824,134.00, ikiwa ni asilimia 117 ya lengo.

**Malengo na Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2024/25**

Kwa mwaka wa fedha 2024/25, TRA Mkoa wa Ruvuma inatarajiwa kukusanya shilingi 41,499,983,492.93, ambapo hadi Desemba 2024, TRA ilikusanya shilingi 24,164,946,699.86, sawa na asilimia 109 ya lengo.

Makusanyo ya kila mwezi yalikuwa kama ifuatavyo:

- Julai 2024: 3,474,388,415.19 (asilimia 112 ya lengo)
- Agosti 2024: 3,714,749,189.60 (asilimia 106 ya lengo)
- Septemba 2024: 4,336,745,569.51 (asilimia 108 ya lengo)
- Oktoba 2024: 3,715,478,139.43 (asilimia 103 ya lengo)
- Novemba 2024: 3,663,406,097.67 (asilimia 103 ya lengo)
- Desemba 2024: 5,260,179,288.46 (asilimia 120 ya lengo)

Jumla ya makusanyo kwa kipindi hicho ni shilingi 24,164,946,699.86, ikiwa ni asilimia 109 ya lengo.

**Maendeleo ya Miundombinu**

TRA Ruvuma imefanikiwa kukarabati majengo ya ofisi za Mkoa na Wilaya ya Tunduru, pamoja na ujenzi wa nyumba za watumishi katika kituo cha forodha cha Mkenda Nakawale, ambazo zimekamilika kwa asilimia 98.

**Mikakati ya Kuboresha Ukusanyaji wa Kodi**

1. Kuongeza elimu kwa wafanyabiashara kuhusu kodi.
2. Kusimamia uwasilishaji wa ritani na malipo kwa wakati.
3. Kusimamia matumizi ya EFD kwa ukaguzi wa mara kwa mara.
4. Kufuatilia biashara ya magendo mipakani.
5. Kushirikiana na wadau wa biashara kama TCCIA.

Mamlaka ya Mapato Mkoa wa Ruvuma inaendelea kufanya jitihada kubwa kuhakikisha ukusanyaji wa mapato unaimarika.

Tunamshukuru Mheshimiwa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan kuweka mazingira bora ya biashara na kusaidia kuongeza makusanyo ya kodi nchini.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ameshiriki mwaka huu katika maadhimisho ya utoaji tuzo kwa walipakodi bora mkoani Ruvuma,

Kanali Abbas ameipongeza TRA kwa juhudi zake katika kuhamasisha ulipaji wa kodi stahiki, na kuwashukuru wafanyabiashara kwa kujitolea katika kutoa michango ya kodi.

Katika hafla hiyo, Kanali Abbas alisema wafanyabiashara hao wameonesha uzalendo kwa Taifa na kuwaomba waendelee kuwa mabalozi wazuri kwa wengine ili waweze kujifunza kutoka kwao.

Amesisitiza umuhimu wa uhusiano mzuri kati ya Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na wafanyabiashara kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi.

TANZANIA RURAL AND URBAN ROADS AGENCY
TARURA
Improved Roads For Sustainable Development



**Mradi wa daraja la Njoka wilayani Songea lenye urefu wa mita 20**

# MAFANIKIO TARURA

"Tunachukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio haya makubwa katika sekta ya miundombinu. Kupitia ongezeko la fedha kupitia Mfuko wa Majimbo na Tozo za mafuta, wananchi wa Ruvuma wamefaidika na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, jambo ambalo limewezesha usafiri wa haraka na rahisi wa mazao na huduma nyingine.



Rais Dkt Samia Suluhu Hassan



**Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silivester Chinengo akiwa ofisini kwake mjini Songea.**




**MAWASILIANO**
**TUNDURU ROAD, 57180 S.L.P 74, SONGEA, RUVUMA, Regional Commissioner Office**
**Telephone: 0252602256**
**Mobile: 0252602256 · Fax: 0252602144**


***"Tunakufungulia Barabara kufika Kusiko Fikika"***

MAFANIKIO TARURA Improved Roads For Sustainable Development

# Mafanikio ya miaka minne ya Rais Samia katika utekelezaji wa miradi ya barabara Ruvuma

Na ALBANO MIDELO

Mkoa wa Ruvuma kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), umekamilisha kwa kiwango kikubwa utekelezaji wa miradi ya barabara katika kipindi cha miaka minne ya utawala wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silvester Chinengo anasema TARURA Mkoa wa Ruvuma ina mtandao wa barabara wa kilometa 7146.202, ambapo asilimia 32.36 ya hizo ni barabara za Mjazio (Feeder Roads), asilimia 53.85 ni za Mkusanyo (Collector Roads), na asilimia 13.43 ni za Jamii/ Kijiji (Community Roads).



Mradi wa ujenzi wa barabara ya lami Matomondo - JKT Mlale wilayani Songea ambao TARURA wameukamilisha kilometa sita kwa kiwango cha lami

**Hali ya Barabara Kabla ya Nyongeza ya Bajeti**

Kabla ya nyongeza ya bajeti, hali ya barabara katika Mkoa wa Ruvuma ilikuwa duni. Kilometa 890.449 za barabara zilikuwa za changarawe (12.46%), kilometa 93.635 zilikuwa za barabara za lami (1.31%) na kilometa 6159.19 zilikuwa za udongo (86.19%).

Kwa mujibu wa Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma, Barabara zilizokuwa zinapitika kwa mwaka mzima zilikuwa asilimia 12.46, na kwamba barabara nzuri zilikuwa ni kilometa 1391.453, za hali ya kuridhisha kilometa 1572.083, na barabara zilizokuwa katika hali isiyoridhisha ni kilometa 4182.667.

**Hali ya Barabara Baada ya Nyongeza ya Bajeti**

Meneja huyo wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Chinengo anasema baada ya nyongeza ya bajeti kutoka kwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, hali ya barabara katika Mkoa wa Ruvuma ilianza kuboreka.

Anasema hivi sasa, barabara za changarawe zimefika kilometa 1372.581, barabara za lami ni kilometa 118.635 na barabara za zege kilometa 6.92.

Amezitaja barabara zinazopitika kwa mwaka mzima zimeongezeka hadi asilimia 71.87 sawa na kilometa 5136.258 na kilometa. 2009.93 sawa na asilimia 28.13 na zinapitika kwa msimu.

Hata hivyo, anabainisha zaidi kuwa madaraja, makalavati na drifti vimeongezeka kutoka 471, 1940 na 63 hadi 511, 2130, na 633 mtawalia.



> "Barabara zinazopitika kwa mwaka mzima zimeongezeka hadi asilimia 35 na kwamba barabara zenye hali nzuri zimefika kilometa 2250.387, zenye hali ya kuridhisha 1767.899, na zile zilizoko katika hali isiyoridhisha ni kilometa 3127.913.

**Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silivester Chinengo**

**Hali ya Utekelezaji Kabla ya Nyongeza ya Bajeti**

Kulingana na Mhandisi Chinengo, kabla ya nyongeza ya bajeti, utekelezaji wa miradi ya barabara ilikuwa ndogo na ilitumika kutengeneza barabara na madaraja madogo.

Anasema kwa mwaka wa fedha wa 2020/2021, bajeti ya Mfuko wa Barabara ilikuwa Tsh 7,972,808,764.84, ambapo ilitumika katika matengenezo ya barabara na ujenzi wa madaraja madogo na mifereji.

**Hali ya Utekelezaji Baada ya Nyongeza ya Bajeti**

Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Silvester Chinengo anasema kuanzia mwaka wa fedha 2021/2022, Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan aliona umuhimu wa kuongeza bajeti katika sekta ya miundombinu ya barabara.

"Bajeti ya barabara kwa mkoa wa Ruvuma ilipata nyongeza kubwa kupitia Tozo ya mafuta ya petroli na dizeli na Mfuko Mkuu wa Serikali kwa fedha za majimbo'," anasema.

Anabainisha kuwa kwa mwaka wa fedha 2021/2022, jumla ya bajeti ilifikia TZS 20,166,151,320.89, huku kwa mwaka wa 2022/2023 ikifika TZS 23,757,962,850.44, na kwa mwaka wa fedha 2023/2024 TZS 20,965,608,008.53 na Kwa mwaka wa fedha wa

*"Tunakufungulia Barabara kufika Kusiko Fikika"*

MAFANIKIO TARURA

# Mafanikio ya miaka minne ya Rais Samia katika utekelezaji wa miradi ya barabara Ruvuma



**Baadhi ya barabara na madaraja yaliyotengenezwa na TARURA wilayani Tunduru**

2024/2025, bajeti ilifikia TZS 38,394,647,987.76.

Anasisitiza kuwa katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, Mkoa wa Ruvuma umetumia sh. bilioni 103.2 kwa matengenezo ya barabara na madaraja.

Anasema hivi sasa, barabara nyingi zimeboreshwa, ikiwa ni pamoja na barabara za changarawe, lami na barabara za zege na kwamba madaraja 60, mifereji mita 5,100 na barabara mpya kilometa 125.03 zimejengwa.

**Miradi ya Kimkakati inayotekelezwa Kutokana na Ongezeko la Bajeti**

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Rais Samia, miradi muhimu imefanyiwa kazi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa barabara ya Luhindo-Mpepo-Darpori kwa kiwango cha changarawe, ujenzi wa barabara za ufukwe wa Ziwa Nyasa kwa ajili ya kuhamasisha utalii, na barabara mpya za Kilosa na Mbamba Bay ambazo zitaongeza vivutio vya utalii katika Wilaya ya Nyasa.

**Mikakati Iliyopangwa Kuendeleza Uboreshaji wa Barabara**

Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma anaitaja Mikakati ya kuendeleza barabara katika Mkoa wa Ruvuma kuwa ni pamoja na ujenzi wa madaraja na makalavati, ujenzi wa barabara za lami, ufunguzi wa barabara mpya katika maeneo ya uwekezaji mkubwa wa kilimo na uchimbaji madini, uboreshaji wa barabara za mitaa na uwekaji wa taa za barabarani katika maeneo mbalimbali.

**Pongezi kwa Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan**

"Tunachukua fursa hii

**BILIONI 103.2**

Ni kiasi cha fedha kilichotumika kutengeneza barabara na madaraja katika kipindi cha miaka minne ya Rais Samia Mkoa wa Ruvuma.



**Daraja lililojengwa kwa teknolojia ya mawe katika mto Mgombezi linalounganisha kijiji cha ipupuma,Mgombezi na Chechengu katika Halmashauri ya Madaba wilayani Songea.**

***"Tunakufungulia Barabara kufika Kusiko Fikika"***

# Mafanikio ya miaka minne ya Rais  Samia katika utekelezaji wa miradi ya barabara Ruvuma

kumpongeza Mheshimiwa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan kwa mafanikio haya makubwa katika sekta ya miundombinu. Kupitia ongezeko la fedha kupitia Mfuko wa Majimbo na Tozo za mafuta, wananchi wa Ruvuma wamefaidika na uboreshaji wa miundombinu ya barabara, jambo ambalo limewezesha usafiri wa haraka na rahisi wa mazao na huduma nyingine," anasema Meneja wa TARURA Mkoa wa Ruvuma kwa niaba ya wananchi.



Mwonekano wa Barabara mpya Kihamili-Hospitali ya Halmashauri ya wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma inayojengwa kwa kiwango cha lami na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini Tanzania (TARURA).



Mwonekano wa daraja lililojengwa na Tarura katika barabara ya Tunduru Sekondari wilayani Tunduru



Mradi wa ujenzi wa barabara za lami katika mitaa ya mji wa Namtumbo

*"Tunakufungulia Barabara kufika Kusiko Fikika"*

# MAFANIKIO SOUWASA



Mradi wa maji wa Pambazuko Kata ya Mletele Manispaa ya Songea ambao umetekelezwa kwa asilimia 100 na kuanza kuhudumia wananchi.



Ujenzi wa tanki kubwa la kuihifadhia maji kwenye mradi mkubwa wa maji wa miji 28 unaotekelezwa katika Manispaa ya Songea kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 145.



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed akizungumza baada ya kukagua mradi mkubwa wa maji wa miji 28 unaotekelezwa mjini Songea




Mkurugenzi wa SOUWASA Mhandisi Patrick Kibasa akiwa ofisini kwake mjini Songea




## MAWASILIANO

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea
S.L.P 363, Songea, Mtaa wa **Mahenge Simu:** 025 260 2326.
**Simu ya bure:** 0800 110010.
www.souwasa.go.tz.

MAFANIKIO SOUWASA






**Ujenzi wa tanki kubwa la kuihifadhia maji kwenye mradi mkubwa wa maji wa miji 28 unaotekelezwa katika Manispaa ya Songea kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 145**

# RAIS SAMIA ALIVYODHAMIRIA KUMALIZA KERO YA MAJI MANISPAA YA SONGEA

**Na ALBANO MIDELO**

Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, akiwa anatimiza miaka minne ya uongozi wake, ameendelea kuonesha dhamira yake ya dhati ya kuboresha huduma za maji, hususan katika miji ya Tanzania.

Mji wa Songea, mkoani Ruvuma, ni mojawapo ya maeneo ambayo yananufaika kwa kiasi kikubwa na juhudi hizo,

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa, anasema katika kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Songea, Rais Samia, ametoa shilingi 145,773,015,609.69 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa kimkakati.

Anabainisha kuwa mradi huo unahusisha miji 28 na unalenga kuongeza uzalishaji wa maji na kuboresha miundombinu ya huduma za maji kuhakikisha kuwa wananchi wanapata huduma hiyo kwa urahisi na kwa wakati.

"Hadi sasa mkandarasi aliyepewa tenda ya kutekeleza mradi huu amepokea kiasi cha shilingi 21,865,952,341.45 kama fedha za awali na utekelezaji umefikia asilimia tano huku kazi ikiendelea kwa kasi'," anasema Mhandisi Kibasa.

Anasema mradi huo unatarajiwa kunufaisha wakazi 619,195 wa Manispaa ya Songea ifikapo mwaka 2045 na hivyo kumaliza changamoto ya upatikanaji wa maji safi na salama katika eneo hilo.

Hata hivyo, anabainisha kuwa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) inasimamia utekelezaji wa mradi huo, kwa kushirikiana na wizara ya maji na mkandalasi anatarajia kupokea fedha zaidi kuhakikisha utekelezaji wa mradi unafanikiwa kama ilivyopangwa.

Kwa upande mwingine katika kipindi cha uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, SOUWASA inatekeleza miradi mbalimbali ya maji katika Manispaa ya Songea.

Anabainisha kuwa miradi imetekelezwa kwa mafanikio makubwa kutokana na juhudi za serikali katika kutoa fedha na usimamizi wa karibu wa miradi hiyo.

Katika Ilani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ya mwaka 2020-2025, serikali ilijizatiti kufikisha huduma ya maji safi na salama kwa asilimia 95 mijini na 85 vijijini na tayari utekelezaji umeonesha mafanikio katika Manispaa ya Songea.

Mkurugenzi wa SOUWASA anabainisha kuwa Rais Dkt. Samia ametoa shilingi 4,822,204,847.10 kwa ajili ya miradi ya maji ya Manispaa ya Songea, ambapo SOUWASA imepokea fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maji.

Anasema hadi sasa, miradi mingi imetekelezwa kwa mafanikio makubwa ikiwemo mradi wa ujenzi wa maji safi katika maeneo ya Lilambo A na Lilambo B, ambapo gharama za



Katika kuboresha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika Manispaa ya Songea, Rais Samia , ametoa kiasi cha fedha cha Shilingi 145,773,015,609.69 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi mkubwa wa maji wa kimkakati.

**Mkurugenzi wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Songea (SOUWASA) Mhandisi Patrick Kibasa.**



MAFANIKIO SOUWASA

# RAIS SAMIA ALIVYODHAMIRIA KUMALIZA KERO YA MAJI MANISPAA YA SONGEA

mradi ni shilingi 855,545,306.10 na kwamba mradi umekamilika kwa asilimia 100 na kunufaisha watu 4,934.

Mradi mwingine ni ujenzi wa maji safi eneo la Pambazuko katika Manispaa ya Songea, wenye gharama ya shilingi 579,832,648.00 ambao umekamilika kwa asilimia 100 na kuwanufaisha watu 3,390.

Kwa mujibu wa Mhandisi Kibasa mradi mwingine ni ujenzi wa maji safi katika eneo la Viwanda Lilambo, ambapo gharama za mradi ni shilingi 415,980,885.00 na viwanda 200 vinanufaika na mradi huu.

Mkurugenzi wa SOUWASA anautaja mradi mwingine kuwa upanuzi wa maji safi katika eneo la Luwawasi, uliogharamu shilingi 329,127,960.00, ambao umekamilika kwa asilimia 100 na kuwanufaisha watu 7,993.

Anasema utekelezaji wa miradi hiyo umeleta mafanikio makubwa ambapo huduma ya maji safi na salama katika Manispaa ya Songea imeongezeka kutoka asilimia 84 Machi 2021 hadi asilimia 90 Desemba 2024.

Hata hivyo, anasema SOUWASA inatarajiwa kuendelea kuboresha zaidi huduma za maji kutokana na mafanikio makubwa ya Rais Dkt.Samia katika kuboresha sekta ya maji nchini, huku wananchi wa Songea wakinufaika moja kwa moja na miradi hiyo.

Kwa ujumla, serikali ya Rais Dkt. Samia inaendelea kuonesha dhamira ya kuhakikisha kwamba huduma za maji zinapatikana kwa urahisi kwa wananchi mijini na vijijini nchini.


Miradi ya maji inayotekelezwa katika Manispaa ya Songea ni mfano mzuri wa juhudi za serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi na kuleta maendeleo endelevu katika maeneo ya kipaumbele.



Ujenzi wa tanki la kuhifadhia maji kwenye mradi mkubwa wa maji wa miji 28 unaotekelezwa katika Manispaa ya Songea kwa gharama ya zaidi ya shilingi bilioni 145



Mradi wa maji wa Pambazuko Kata ya Mletele Manispaa ya Songea ambao umetekelezwa kwa asilimia 100 na kuanza kuhudumia wananchi



MRADI wa Sekondari ya Jenista Mhagama yenye kidato cha kwanza hadi cha sita iliyojengwa Parangu Peramiho ni miongoni mwa shule ambazo serikali imeweka uwekezaji mkubwa

# SONGEA DC YAPIGA HATUA KUBWA KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO

**Na ALBANO MIDELO**

Katika kipindi cha miaka mitano, Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, imepiga hatua kubwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia mabilioni ya shilingi kwa ajili ya kuboresha huduma za jamii na miundombinu.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Songea Elizabeth Gumbo anasema katika utekelezaji wa miradi, halmashauri imetumia zaidi ya shilingi **54.22 bilioni** kati ya mwaka wa fedha 2020-2021 na 2024-2025. Miradi hii inahusisha sekta mbalimbali kama afya, elimu, maji, barabara na kilimo.

**Utekelezaji wa Miradi kwa Miaka Tano**

Katika mwaka wa fedha **2020-2021**, halmashauri ilitumia takribani **TZS 5.1 bilioni** kwa miradi ya maendeleo. Fedha hizo zilielekezwa zaidi katika kuboresha miundombinu ya shule, vituo vya afya na barabara.

Kwa mwaka **2021-2022**, matumizi yaliongezeka hadi **TZS 10.26 bilioni**, ambapo miradi mingi ilihusisha ujenzi wa madarasa, upanuzi wa vituo vya afya na usambazaji wa maji safi vijijini.

Mwaka **2022-2023** uliona ongezeko zaidi, huku kiasi cha **TZS 12.94 bilioni** kikitumiwa kuboresha huduma za msingi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hospitali za wilaya na maboresho ya sekta ya kilimo kwa wakulima wadogo.

Kwa mwaka **2023-2024**, matumizi yalifikia **TZS 9.32 bilioni**, ambapo miradi muhimu ilikuwa ni ujenzi wa barabara za vijijini, maboresho ya shule za msingi na sekondari na miradi ya nishati.

Mwaka wa fedha **2024-2025** umeonesha uwekezaji mkubwa zaidi, kwa kutumia **TZS 16.60 bilioni**, hasa katika miradi mikubwa ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa hospitali, shule mpya na miundombinu ya maji safi.

**Mafanikio na Changamoto**

Kupitia miradi hii, wananchi wa Halmashauri ya Songea wamefaidika kwa kiwango kikubwa kwa kupata huduma bora zaidi, hasa katika sekta za afya na elimu. Hata hivyo, changamoto kama ucheleweshaji wa fedha na gharama kubwa za vifaa zimeathiri utekelezaji wa baadhi ya miradi.

Licha ya changamoto hizo, halmashauri inaendelea kujipanga kuhakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati na kuleta manufaa kwa jamii. Hatua hii ni ushahidi wa juhudi za serikali na wadau wa maendeleo katika kuimarisha ustawi wa wananchi wa Songea DC.



Mwaka **2022-2023** uliona ongezeko zaidi, huku kiasi cha **TZS 12.94 bilioni** kikitumiwa kuboresha huduma za msingi, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa hospitali za wilaya na maboresho ya sekta ya kilimo kwa wakulima wadogo.



MRADI wa ujenzi wa stendi ya mabasi ya Lundusi Peramiho Halmashauri ya Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma ambapo ujenzi unaendelea.



MWONEKANO wa majengo ya Hospitali ya Halmashauri ya Songea iliyojengwa katika Kijiji cha Mpitimbi, ambayo imeanza kuhudumia wananchi.

THE MINING COMMISSION

**CONTACT US**
Resident Mines Officer,
P.O.Box 327, SONGEA
E-mail: ruvuma@tumemadini.go.tz



Soko la madini ya dhahabu na vito la Tunduru lilifunguliwa rasmi na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan Septemba 2024 mjini Tunduru

> "Masoko haya yamesaidia kuimarisha biashara ya madini na kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022 hadi Disemba 2024, jumla ya madini yaliyouzwa katika masoko haya ilikuwa na thamani kubwa ikiwemo madini ya vito na dhahabu.

# MAFANIKIO SEKTA YA MADINI MKOANI RUVUMA INAVYOCHOCHEA UKUAJI WA UCHUMI NCHINI



Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Alphonce Bikulamchi akiwa ofisini kwake mjini Songea



Baadhi ya madini ya makaa ya mawe katika Kampuni ya JITEGEMEE HOLDING katika Halmashauri ya Mbinga yakiwa katika bandari ya nchi kavu yakisubiri kusafirishwa

MAFANIKIO MADINI

# MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA, MADINI YANAVYOUPAISHA MKOA WA RUVUMA



RAIS Dkt Samia Suluhu Hassan akiwa na Waziri wa Madini, Anthony Mavunde (katikati), pamoja na Afisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Alphonce Bikulamchi (kulia), katika Soko la Madini ya Dhahabu na Vito wilayani ya Tunduru.

Na ALBANO MIDELO

PATO la Taifa katika Mkoa wa Ruvuma limeongezeka kutoka shilingi bilioni 2.37 mwaka 2012 hadi bilioni 6.39 mwaka 2022.

Kwa mujibu wa takwimu kutoka Ofisi ya Taifa ya Takwimu (NBS) Pato la Taifa (GDP) katika kanda hiyo limekuwa linaongezeka mwaka hadi mwaka na kufanya kanda hiyo kuchangia wastani wa asilimia 10.5 ya pato la taifa katika mkoa wa Ruvuma.

Kwa mujibu wa NBS ongezeko hilo limechangiwa zaidi na uzalishaji katika shughuli za madini na kilimo

**Uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe Ruvuma**

Uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe katika Mkoa wa Ruvuma umekuwa chanzo kikubwa cha mapato ya serikali ambapo katika mwaka wa fedha wa 2023/2024, serikali imeuza tani 1,356,249.84 za makaa ya mawe zenye thamani ya Dola za Marekani zaidi ya milioni 144.9.

> Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma ilikusanya jumla ya shilingi 105,120,541,415.03, sawa na asilimia 126 ya lengo la makusanyo.



Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Alphonce Bikulamchi, anasema kupitia mauzo hayo serikali imekusanya kiwango cha mrabaha wa Dola za Marekani 3,937,434.98 na ada ya ukaguzi Dola za Marekani 914,034.68 na kwamba madini hayo yameuzwa ndani ya nchi, nchi Jirani, barani Ulaya na Asia kupitia bandari ya Mtwara na Dar es salaam.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2023/2024 Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma, ilipangiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 41 na kwamba katika kipindi cha kuanzia Julai hadi Desemba ofisi hiyo ilikusanya zaidi ya shilingi bilioni 13 sawa na asilimia 64.

Uchimbaji na uuzaji wa makaa ya mawe mkoani Ruvuma ulianza mwaka 2011 kukiwa na kampuni moja ya uchimbaji ya Tancoal Energy ambapo hadi kufikia mwaka 2019 wadau wengi walijitokeza na kufanya uwekezaji mkubwa katika uzalishaji wa madini ya makaa ya mawe.

**Leseni za Uchimbaji na Biashara ya Madini**

Ofisi ya Afisa Madini Mkazi wa Ruvuma imekuwa ikitoa leseni mbalimbali za uchimbaji na biashara ya madini kama vile leseni za uchimbaji mdogo (PML), leseni za madini ya biashara (Dealers na Brokers).

Kwa mujibu wa Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Alphonce Bikulamchi kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022 hadi 2024/2025, idadi ya leseni zilizotolewa zimekuwa zikiongezeka, huku mkoa ukiwa na jumla ya leseni 144 za utafutaji madini na leseni za uchimbaji mkubwa na wa kati.

**Ukusanyaji wa Maduhuli ya Serikali:**

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2021/2022 hadi 2024/2025, Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma ilikusanya jumla ya shilingi 105,120,541,415.03, sawa na asilimia 126 ya lengo la makusanyo.

" Huu ni uthibitisho wa ufanisi katika usimamizi wa makusanyo ya fedha zinazotokana na shughuli za madini, ikichangiwa na ongezeko la mauzo ya madini," anasema Mhandisi Bikulamchi

**Masoko ya Madini:**

Mkoa wa Ruvuma unasimamia masoko mawili ya madini ambayo ni Soko la Madini ya Dhahabu na Vito lililopo Songea Mjini na Soko la Madini ya Vito katika Wilaya ya Tunduru.

Afisa Madini Mkazi Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Alphonce Bikulamchi anasema Masoko haya yamesaidia kuimarisha biashara ya madini na kwa kipindi cha mwaka wa fedha wa 2021/2022 hadi Disemba 2024, jumla ya madini



Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas Ahmed alipotembelea mgodi wa dhahabu wa Goldfield uliopo katika kijiji cha Lukarasi wilayani Mbinga.

THE MINING COMMISSION




soko la madini ya dhahabu na vito la Tunduru ambalo lilifunguliwa rasmi na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan Septemba 2024 mjini Tunduru

Kumekuwepo na ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe kutoka wastani wa tani 1.5 milioni mwaka 2021/2022 hadi tani 2.56 milioni mwaka 2023/2024 ambapo anasisitiza kuwa hiyo ni ishara ya mafanikio katika sekta hii ambayo inatoa ajira na kuongeza mapato ya serikali.

# MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA, MADINI YANAVYOUPAISHA MKOA WA RUVUMA

yaliyouzwa katika masoko yalikuwa na thamani kubwa, ikiwemo madini ya vito na dhahabu.

**Uzalishaji wa Makaa ya Mawe:**

Uchimbaji wa makaa ya mawe katika mkoa wa Ruvuma umeongeza tangu mwaka 2011 na kwa mwaka 2021/2022 hadi 2024/2025, ambapo kiasi cha tani 8,848,176.91 za makaa ya mawe kilikuwa kimeuzwa.

Mhandisi Bikulamchi anasema kutokana mauzo hayo Serikali ilikusanya shilingi 78,797,933,654.78 kupitia mrabaha na ada za ukaguzi na kwamba biashara ya makaa ya mawe imechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa mkoa.

Meneja Uchimbaji wa kampuni ya Mgodi wa Makaa ya Mawe ya JITEGEMEE wilayani Mbinga mkoani Ruvuma Bosco Mabena anasema malori zaidi ya 120 hubeba makaa ya mawe kwa siku katika mgodi huo na kwamba uzalishaji wa madini hayo unafanyika kwa njia za kisasa.

Mabena anasema makaa ya mawe yanayozalishwa kwenye mgodi wa Kampuni ya JITEGEMEE hutumika katika viwanda vilivyopo ndani ya nchi, Afrika Mashariki na nchi za Ulaya na China.

"Huu ni mgodi wa kitanzania ambao unaendeshwa na wazawa kwa asilimia 100, tunavyo vitalu vya makaa ya mawe ambavyo vinachimba makaa ya mawe kwa njia ya kisasa kwa sababu tuna vifaa vya kisasa vikiwemo maabara ya kisasa na mitambo ya kuchakata makaa ya mawe kwa ubora wa hali ya juu," alisisitiza Mabena.

Anasema makaa ya mawe yanatumika katika viwanda mbalimbali vikiwemo vya saruji katika mikoa mbalimbali nchini, pia anasema makaa ya mawe yanatumika katika viwanda vya tires, nondo na viwanda vyote vidogo vidogo



Baadhi ya madini ya makaa ya mawe katika Kampuni ya JITEGEMEE HOLDING katika Halmashauri ya Mbinga yakiwa katika bandari ya nchi kavu ili kusafirishwa

Serikali ilikusanya shilingi 78,797,933,654.78 kupitia mrabaha na ada za ukaguzi na kwamba biashara ya makaa ya mawe imechangia kwa kiasi kikubwa katika ukuaji wa uchumi wa mkoa.

THE MINING COMMISSION

# MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA, MADINI YANAVYOUPAISHA MKOA WA RUVUMA



**Waziri Mkuu Mheshimiwa Kassim Majaliwa alipotembelea na kukagua Mgodi wa Makaa ya Mawe wa Jitegemee Holding uliopo Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma**

vikiwemo viwanda vya nguo ambapo anasema wanapakia makaa ya mawe bandari ya nchi kavu zaidi ya 120 kwa siku.

Hata hivyo anasema Kampuni ya JITEGEMEE ina ghala la kutunzia makaa ya mawe katika bandari ya Mtwara lenye uwezo wa kutunza makaa ya mawe zaidi ya tani laki tano kwa ajili ya kuuza katika masoko ya nje ya nchi kupitia bandari ya Mtwara.

**Mafanikio ya Sekta ya Madini:**

Sekta ya madini mkoani Ruvuma imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.

Mhandisi Bikulamchi anayataja baadhi ya mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na ongezeko la makusanyo ya maduhuli kutoka wastani wa shilingi bilioni 21.6 mwaka 2021/2022 hadi kufikia shilingi bilioni 30 mwaka 2023/2024.

Anasema kumekuwepo na ongezeko la mauzo ya makaa ya mawe kutoka wastani wa tani 1.5 milioni mwaka 2021/2022 hadi tani 2.56 milioni mwaka 2023/2024 ambapo anasisitiza kuwa hiyo ni ishara ya mafanikio katika sekta hii ambayo inatoa ajira na kuongeza mapato ya serikali.

Sekta ya madini mkoani Ruvuma inaendelea kuimarika na kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa mkoa na taifa. Uwekezaji wa ziada, usimamizi mzuri wa masoko, na ongezeko la makusanyo ya maduhuli ni baadhi ya mafanikio yanadhihirisha ukuaji wa sekta hii.

Dhamira ya serikali ya Awamu ya Sita ya kuanzisha masoko ya kisasa ya madini na ongezeko la idadi ya migodi, kunaufanya mkoa wa Ruvuma kuendelea kuwa kivutio kwa wawekezaji hivyo kuwa chanzo na mapato kwa serikali.

Biashara ya madini ya makaa ya mawe mkoani Ruvuma ilishamiri baada ya mauzo jumla ya makaa ya mawe ya tani 450,675.32 ndani ya nchi na tani 1,060,699.05 ziliuzwa nje ya nchi katika kipindi cha Julai hadi Desemba 2022.

Mwaka 2019 wadau wengi walijitokeza na kufanya uwekezaji katika shughuli za Makaa ya Mawe hali iliyosababisha kuongezeka kwa uzalishaji wa madini hayo kuanzia mwaka 2020.

Uzalishaji wa Madini ya Makaa ya Mawe mkoani Ruvuma unatoa mchango mkubwa kwenye maduhuli yanayokusanywa na Tume ya Madini mkoani Ruvuma.

Katika kipindi cha hivi karibuni, Makaa ya Mawe yamekuwa yakihitajika ulimwenguni kama chanzo cha nishati na hivyo kuwa moja ya chanzo kikubwa cha mapato ya Serikali.

Katika mwaka wa fedha 2021/2022, Ofisi ya Madini Mkoa wa Ruvuma ilipangiwa kukusanya maduhuli ya serikali Shilingi bilioni 12. Hata hivyo hadi kufikia Juni 30,2022, Ofisi ya Madini Ruvuma ilikuwa imekusanya cha shilingi bilioni 21, sawa na asilimia 179 ya lengo la mwaka huo.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, Ofisi ya Madini Ruvuma ilipangiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 26 hadi kufikia Desemba 31,2022,Ofisi

**MAFANIKIO**

***Sekta ya madini mkoani Ruvuma imekuwa na mchango mkubwa katika uchumi wa mkoa na taifa kwa ujumla.***



# MAFANIKIO YA MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA, MADINI YANAVYOUPAISHA MKOA WA RUVUMA




**"Utafiti uliofanywa Mwaka 2001, kwenye mgodi wa Ngaka wilayani Mbinga ulibaini kuwepo kwa madini ya makaa ya mawe yanayoongoza kwa ubora duniani kiasi cha tani milioni 400.**

**Meneja Uchimbaji madini ya makaa ya mawe kampuni ya Jitegemee Bosco Mabena.**

ya Madini Ruvuma ifanikiwa kukusanya zaidi ya shilingi bilioni 19 sawa na asilimia 75.25 ya lengo.

Madini ya makaa ya mawe yanayochimbwa Ruvuma, huuzwa ndani ya nchi zinazotuzunguka barani Ulaya na Asia kupitia bandari za Mtwara na Dar es Salaam.

**Shughuli za utafiti wa makaa ya mawe Ruvuma**

Shughuli za utafiti na uchimbaji wa makaa ya mawe katika mkoa wa Ruvuma zinafanyika katika Wilaya ya Mbinga maeneo ya Mbalawala, Buyula, Paradiso, Ntunduwaro, Amanimakoro na Ngaka, katika wilaya ya Songea katika maeneo ya Muhukuru, Mdunduwalo, Njuga na Kikunja na Wilaya ya Nyasa maeneo ya Malini.

Waziri Mkuu wa Tanzania Mheshimiwa Kassim Majaliwa alitembelea na kukagua mgodi wa makaa ya mawe wa Kampuni ya Jitegemee katika Kijiji cha Ntunduwaro wilayani Mbinga ambapo aliridhishwa kutokana na kushamiri kwa biashara hiyo.

Waziri Mkuu alifurahishwa na biashara ya makaa ya mawe baada ya kutembelea mgodi wa Jitegemee ambapo alielezwa mgodi umetoa ajira za kudumu 85, ajira za muda 150 ambapo alisema hiyo ni faida kubwa kwa wananchi na serikali ambayo inapata mapato makubwa kutokana na kodi na tozo mbalimbali.

Utafiti umebaini kuwa Mkoa wa Ruvuma una hazina ya makaa ya mawe zaidi ya tani milioni 227 ambazo zinatarajiwa kuchimbwa kwa miaka 300.

Utafiti uliofanywa mwaka 2001, kwenye mgodi wa Ngaka wilayani Mbinga ulibaini kuwepo kwa madini ya makaa ya mawe yanayoongoza kwa ubora duniani kiasi cha tani milioni 400.

Tafiti za awali za makaa ya mawe zimefanyika katika maeneo ya Mbalawala Mbinga ambako imebainika kuwa na tani milioni 99.5, Mbuyula Mbinga tani milioni 15.1 na Muhukuru Songea tani milioni 27.

Utafiti mwingine umefanyika katika eneo la Njuga wilaya ya Songea ambako kuna tani milioni 23, wilaya ya Nyasa maeneo ya Malini kata ya Mtipwili tani milioni 29, kijiji cha Liweta Kata ya Mbaha tani milioni 34.

Ubora wa makaa ya mawe yanayopatikana kwenye maeneo hayo yana wastani wa Calorific Value (CV) 5,000 hadi 7,000, hata hivyo uchimbaji mkubwa wa makaa ya mawe unafanyika katika maeneo ya Mbalawala, Mbuyula, Mbambabay, Muhukulu na Liweta.



**Jengo la Ofisi ya Madini mkoa wa Ruvuma**

RUWASA
Rural Water Supply and Sanitation Agency
"Maji Bombani"

# MAFANIKIO RUWASA



**RAIS Dkt.Samia Suluhu Hassan alipoweka jiwe la msingi katika mradi wa maji Mtyangimbole Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, kushoto ni Waziri wa Maji Mheshmiwa Jumaa Aweso**



**Meneja wa RUWASA Mkoa wa Ruvuma Mhandisi Rebman Ganshonga.**

## MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA ILIVYOWATUA NDOO KICHWANI WANANCHI WA RUVUMA

Serikali kupitia RUWASA inatekeleza miradi mbalimbali ya maji katika wilaya zote za Ruvuma, ikiwa ni pamoja na miradi wa maji ya Lipaya unaotekelezwa kwa shilingi bilioni 1.9, Mtyangimbole shilingi bilioni 5.56 na Ndelenyuma shilingi bilioni 1.6.



**MWANANCHI wa Kijiji cha Ngumbo wilayani Nyasa, akifurahia huduma ya maji baada ya serikali kutekeleza mradi wa maji wa Ngumbo**

WASILIANA NASI

P.O BOX 200 SONGEA
0716955190
ruvumarm@ruwasa.go.tz

# MIAKA MINNE YA RAIS SAMIA ILIVYOWATUA NDOO KICHWANI WANANCHI WA RUVUMA




**MRADI wa maji wa Ngumbo Halmashauri ya Nyasa**

**Na ALBANO MIDELO**

Maji ni uhai, na kwa wakazi wa Mkoa wa Ruvuma, uhai huo unazidi kuchanua kwa kasi kupitia miradi mbalimbali ya maji inayoendelea kutekelezwa chini ya Wakala wa Maji Vijijini (RUWASA).

Kwa miongo mingi, wanawake na watoto wa mkoa huu walilazimika kutembea umbali mrefu kubeba ndoo za maji kichwani.

Leo hii, ndoto ya kumtua mwanamke ndoo kichwani inazidi kuwa halisi kupitia juhudi zinazofanywa na serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

**Nguvu ya Bilioni 42.5 kwa Uhai Mpya Ruvuma**

Serikali imetenga jumla ya shilingi bilioni 42.5 kwa ajili ya miradi 35 ya maji katika Mkoa wa Ruvuma. Miradi mikubwa inayotekelezwa kupitia RUWASA ni ule wa Lituhi na Liuli yenye thamani ya shilingi bilioni 11.3, ambao utahudumia wakazi zaidi ya 52,285 waishio vijijini.

Katika mwaka wa fedha 2022/2023, serikali ilitenga shilingi bilioni 28.7 kwa ajili ya miradi ya maji, huku mwaka wa 2023/2024 ukiwa na bajeti ya shilingi bilioni 26.2 kwa lengo la kuboresha upatikanaji wa maji safi na salama.

**Mustakabali wa Miradi ya Maji Ruvuma**

Serikali kupitia RUWASA inatekeleza miradi mbalimbali ya maji katika wilaya zote za Ruvuma, ikiwa ni pamoja na Miradi wa maji ya Lipaya unaotekelezwa kwa shilingi bilioni 1.9, Mtyangimbole shilingi bilioni 5.56, na Ndelenyuma shilingi bilioni 1.6.

> "Kwa miaka mingi, wanawake na watoto tulikuwa tukiteseka, lakini sasa hali imebadilika.

Miradi mingine ni wilayani Mbinga Miradi ya Kipololo shilingi milioni 400 na Kigonsera shilingi milioni 300.

Katika wilaya ya Nyasa Miradi mkubwa wa maji ikiwemo Ng'umbo shilingi bilioni 2.5 na mradi wa Lituhi shilingi bilioni 6.5. na katika wilaya ya Tunduru Mradi wa Misechela wenye thamani ya shilingi bilioni 3.

**Wananchi wanavyonufaika na huduma ya maji**

Stella Mhagama, mkazi wa Kijiji cha Lipaya wilayani Songea, anatoa shukrani kwa serikali kwa utekelezaji wa mradi wa maji ambao umewaondolea adha ya kutembea umbali mrefu kusaka maji.

"Kwa miaka mingi, wanawake na watoto tulikuwa tukiteseka, lakini sasa hali imebadilika," anasema kwa furaha Stella Mhagama.

Katika Wilaya ya Mbinga, Romanus Ndunguru kutoka Kijiji cha Utili anaeleza jinsi mradi wa maji wa shilingi milioni 428 ulivyobadili maisha yao.

Diwani wa Kata ya Mpitimbi wilayani Songea, Mheshimiwa Issa Kindamba, anaeleza kuwa mradi wa maji wa Lipaya umeokoa muda na kupunguza magonjwa yatokanayo na matumizi ya maji yasiyo salama

Ilani ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2020, inalenga asilimia 95 ya upatikanaji wa maji mijini na asilimia 85 vijijini.

Hakuna ubishi kuwa serikali ya Awamu ya Sita inaandika historia mpya katika sekta ya maji. Wananchi wa Ruvuma sasa wanajivunia maendeleo yanayokwenda kumaliza kero maji.



**MRADI wa maji Kijiji cha Lipaya Halmashauri ya Wilaya ya Songea.**



**MRADI wa maji Kata ya Tingi wilayani Nyasa.**

MANTRA TANZANIA ROSATOM



MKUU wa Mkoa wa Ruvuma Kanali Ahmed Abbas akiwa na baadhi ya watendaji waandamizi wa Kampuni ya Mantra Tanzania Limited alipotembelea mradi wa Mto Mkuju uliopo Likuyuseka wilayani Namtumbo.

# MAFANIKIO YA MANTRA TANZANIA LIMITED

## MADINI YA URANI NAMTUMBO: NEEMA MPYA KWA UCHUMI WA TANZANIA

Kampuni ya Mantra Tanzania Limited, mojawapo ya waendeshaji wakuu wa mradi wa urani Namtumbo, imekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza sekta hii. Serikali, kwa upande wake, imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji kupitia sera za madini na kodi zinazovutia wawekezaji.

Mradi huu utakapoanza kutekelezwa, Tanzania inaweza kuwa miongoni mwa wazalishaji wakuu wa madini ya urani...

**MAWASILIANO:**
2nd floor, Masaki Ikon,
Bains Avenue, Masaki
P O BOX 23451 Dar es salaa
TEL +255 764 700 440
EMAIL : mantra@uranium1.co.tz
Www.mantratanzania.co.tz

MANTRA TANZANIA ROSATOM

# MADINI YA URANI NAMTUMBO:
## NEEMA MPYA KWA UCHUMI WA TANZANIA

Na ALBANO MIDELO

KATIKA ukanda wa mikoa ya kusini mwa Tanzania, Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma, imegeuka kuwa kitovu cha mjadala mkubwa wa maendeleo ya madini.

Madini ya urani, mojawapo ya rasilimali muhimu kwa uzalishaji wa nishati ya nyuklia, yamegunduliwa kwa wingi katika eneo la Mto Mkuju. Hii si tu habari njema kwa wawekezaji bali pia kwa Tanzania, kwani mradi huu unatarajiwa kuchochea ukuaji wa uchumi wa taifa.

**Tanzania: Nyumba ya Utajiri wa Madini ya Urani**

Tanzania imebarikiwa na hazina kubwa ya madini ya urani, jambo linaloifanya kuwa kivutio kwa wawekezaji wa kimataifa.

Kampuni ya Mantra Tanzania Limited, mojawapo ya waendeshaji wakuu wa mradi wa urani Namtumbo, imekuwa mstari wa mbele katika kuendeleza sekta hii. Serikali, kwa upande wake, imeweka mazingira mazuri ya uwekezaji kupitia sera za madini na kodi zinazovutia wawekezaji.

Pamoja na utajiri wa rasilimali hii, Tanzania pia itanufaika na miundombinu bora itakayotumika kuwezesha usafirishaji wa madini haya. Bandari ya Dar es Salaam ni lango muhimu la kusafirisha madini haya kwenda masoko ya kimataifa, huku vyuo vikuu na taasisi za mafunzo ya ufundi vikitoa wataalamu wa sekta ya madini.



BAADHI ya watumishi wa kampuni ya Mantra Tanzania Limited wakiwa eneo la mgodi wa madini ya urani.

**Uwekezaji wa Mantra Tanzania Limited na Faida kwa Jamii**

Majani Moremi Wambura, meneja uendelevu wa kampuni ya Mantra Tanzania Limited, anasema Mantra Tanzania Limited haijawekeza tu katika uchimbaji wa urani bali pia katika jamii inayozunguka mgodi huo. Kupitia miradi ya kijamii, kampuni hii imeshirikiana na wakazi wa Vijiji vya Mtonya, Likuyu Seka na Likuyu Mandela ili kuboresha huduma za afya, elimu na ajira. Mafunzo ya usalama kuhusu urani pia yametolewa kwa jamii ili kuhakikisha kuwa wanajua jinsi ya kujikinga dhidi ya hatari zinazoweza kujitokeza.

> Tanzania imejaliwa kuwa na ardhi yenye hazina kubwa ya madini ya urani, jambo lililosababishwa kuanzishwa kwa miradi mbalimbali kama ule wa Mto Mkuju unaoendeshwa na kampuni ya Mantra Tanzania Limited ambayo ni moja ya rasilimali kubwa zaidi za urani ambazo hazijaendelezwa duniani.

**Athari za Mazingira na Hatua za Ulinzi**

Madini ya urani yanahitaji usimamizi makini ili kuhakikisha kuwa uchimbaji wake haudhuru mazingira. Mantra Tanzania Limited imechukua hatua za kuhakikisha kuwa maji yanayotumiwa kwenye uchakataji wa madini haya yanachakatwa upya na kurejeshwa katika mazingira kwa njia salama. Kampuni pia inafanyia tathmini mbinu mpya za uchimbaji rafiki wa mazingira ili kupunguza athari za shughuli zake.

**Tanzania Katika Ramani ya Dunia ya Urani**

Mradi huu utakapoanza kutekelezwa, Tanzania inaweza kuwa miongoni mwa wazalishaji wakuu wa madini ya uraniduniani. Kwa sasa, mradi wa Mkuju unatarajiwa kutoa urani kwa kipindi cha zaidi ya miaka 15, na Tanzania inaweza kuchangia hadi asilimia 4 ya uzalishaji wa urani duniani.

Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Ahmed Abbas Ahmed, ana matumaini makubwa kwamba mradi huu utaiweka Tanzania katika nafasi ya juu katika sekta ya madini duniani.

Madini ya urani Namtumbo si tu fursa kwa wawekezaji, bali ni neema kwa uchumi wa Tanzania. Mradi huu unatoa nafasi za ajira, kuchochea ukuaji wa sekta nyingine kama usafirishaji na elimu, na kuinua viwango vya maisha kwa wakazi wa Namtumbo na maeneo jirani.



WAFANYAKAZI wa Kampuni ya Mantra Tanzania Limited wakiwa na wananchi wa Vijiji vya Likuyu Mandela, Likuyuseka na Matonya ambapo kampuni hiyo itatekeleza mradi huo.

MANTRA TANZANIA LIMITED

# MAFANIKIO NFRA



Muonekano wa vihenge na maghala ya kuhifadhi nafaka katika Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula NFRA Kanda ya Songea eneo la Ruhuwiko mjini Songea

## NFRA SONGEA: NGOME YA USALAMA WA CHAKULA TANZANIA

Katika mwaka wa fedha 2024/25, NFRA Kanda ya Songea ilipangiwa kununua tani 72,000 za mahindi, lakini kufikia Desemba 31, 2024, tayari tani 118,292.057 zilikuwa zimenunuliwa. Ununuzi huu ulifikia asilimia 164.3 ya lengo na kufanya akiba ya mahindi kufikia tani 196,498.737.



# NFRA SONGEA: NGOME YA USALAMA WA CHAKULA TANZANIA



Na ALBANO MIDELO

Katika juhudi za kuhakikisha usalama wa chakula nchini, Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) Kanda ya Songea, imeonesha mafanikio makubwa mwaka wa fedha 2023/24 na 2024/2025.

Kupitia mikakati madhubuti ya ununuzi na uhifadhi wa mahindi, kanda hii imeongeza akiba ya taifa na kusaidia wakulima kupata masoko ya uhakika.

**Songea: Kitovu cha Ununuzi wa Mahindi**

Kanda ya Songea ni miongoni mwa Kanda tisa za NFRA na inategemewa sana kwa uzalishaji wa mahindi kutokana na kilimo kuwa uti wa mgongo wa wananchi wa Mkoa wa Ruvuma.

Katika mwaka wa fedha 2023/24, NFRA ilipanga kununua tani 36,405 za mahindi, lakini juhudi za ununuzi zilileta matokeo ya kuvutia, ambapo tani 79,054.142 zilinunuliwa, ikiwa ni asilimia 217.2 ya lengo. Mahindi haya yaligharimu jumla ya shilingi 59,290,606,500.

**Mikakati ya Ununuzi**

Ili kuhakikisha ufanisi wa ununuzi wa mahindi, NFRA ilitumia njia tatu kuu:

1. **Vituo vya ununuzi vya kudumu na vya muda** - Hii ilihusisha vituo vilivyoanzishwa katika maeneo mbalimbali ili kuwafikia wakulima wengi.

KUPANUA SOKO LA MAHINDI

> Licha ya mpango wa kusafirisha tani 70,000 za mahindi kwenda Zambia, NFRA inapaswa kutafuta masoko zaidi nje ya nchi.

2. **Ushirikiano na vikundi vya wakulima na vyama vya ushirika** - Njia hii ilihimiza ushirikiano wa karibu kati ya wakulima na NFRA.
3. **Kupitia mawakala walioteuliwa** - Wakala wa NFRA waliingia mikataba na wasambazaji wa nafaka kuhakikisha ununuzi unafanyika kwa weledi.

Katika mpango huu, vituo 21 vya ununuzi vilifunguliwa katika Halmashauri saba za Ruvuma, na wakulima waliweza kuuza mazao yao kwa uhakika wa malipo.

**Msimu wa Ununuzi 2024/25: Malengo na Mafanikio**

Katika mwaka wa fedha 2024/25, NFRA Kanda ya Songea ilipangiwa kununua tani 72,000 za mahindi, lakini kufikia tarehe 31 Desemba 2024, tayari tani 118,292.057 zilikuwa zimekwishanunuliwa. Ununuzi huu ulifikia asilimia 164.3 ya lengo, na kufanya akiba ya mahindi kufikia tani 196,498.737.

Bei za ununuzi zilianza kwa shilingi 500 kwa kilo, lakini kutokana na mwitikio mdogo wa wakulima, serikali iliongeza bei hadi shilingi 700, jambo lililoongeza hamasa kwa wakulima na kusababisha msongamano wa mahindi katika vituo vya ununuzi.

**Mwelekeo wa Baadaye: Njia za Kuboresha Sekta ya Hifadhi ya Chakula**

Ili kuboresha zaidi utendaji wa NFRA Songea, hatua zifuatazo zinapaswa kuchukuliwa:

1. **Kukamilisha ujenzi wa vihenge** - Kukamilika kwa mradi wa vihenge 12 na maghala mawili kutasaidia kuongeza uwezo wa kuhifadhi kwa tani 55,000.
2. **Kuboresha miundombinu ya barabara** - Serikali inapaswa kushirikiana na sekta binafsi ili kuboresha barabara zinazoelekea kwenye vituo vya ununuzi.
3. **Kuimarisha mfumo wa ununuzi wa mazao bora** - Programu za mafunzo kwa wakulima kuhusu uhifadhi bora wa mazao zinapaswa kuimarishwa.
4. **Kupanua soko la mahindi** - Licha ya mpango wa kusafirisha tani 70,000 za mahindi kwenda Zambia, NFRA inapaswa kutafuta masoko zaidi nje ya nchi.

Mafanikio ya NFRA Songea ni mfano bora wa namna taasisi za serikali zinavyoweza kusaidia wakulima na kuhakikisha usalama wa chakula.



**MOJA ya mashamba makubwa ya mahindi yaliyopo Kijiji cha Liganga Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.**


# MAFANIKIO MIAKA MINNE CHINI YA RAIS SAMIA



# MRADI WA KABONI

## UNAVYOCHANGIA UHIFADHI NA MAENDELEO YA JAMII

Katika mpango wake wa mwaka 2025, CT Limited imepanga kukamilisha maandiko ya mradi na kuyawasilisha kwa mamlaka husika na kufanikisha uthibitishaji wa mradi na kuuza vyeti vya kaboni ifikapo mwaka 2025/2026.



**BAADHI ya misitu ya asili inayopatikana mkoani Ruvuma.**

# MRADI WA KABONI UNAVYOCHANGIA UHIFADHI NA MAENDELEO YA JAMII

**Na ALBANO MIDELO**

Katika juhudi za kuhifadhi mazingira na kukuza maendeleo ya jamii, kampuni ya Carbon Tanzania (CT Limited) imeibuka kama mdau muhimu katika biashara ya kaboni nchini Tanzania.

Tangu kuanzishwa kwake mwaka 2013, kampuni hii imekuwa ikitekeleza miradi inayolenga kuhifadhi misitu ya asili huku ikitoa faida kwa jamii zinazohusika.

Ofisa wa Mradi wa Carbon Tanzania Ukanda wa Ruvuma Ally Nyenje anasema hivi karibuni, mradi mkubwa wa biashara ya kaboni umeanzishwa katika mkoa wa Ruvuma, ukihusisha jumuiya tano za uhifadhi wa wanyamapori (WMA) zenye jumla ya hekta 856,600 katika Wilaya za Tunduru na Namtumbo.

Kampuni ya Carbon Tanzania (CT Limited) ni kampuni binafsi iliyosajiliwa mwaka 2013 chini ya Sheria ya Makampuni, Nambari 12 ya mwaka 2002 ya S.L.P. 425 ARUSHA.

Kampuni hii inafanya shughuli za uhifadhi wa misitu ya asili kwa lengo la kufanya biashara ya kaboni kwa kuzingatia Kanuni za Biashara ya Kaboni za Tanzania, 2022 na marekebisho yake ya mwaka 2023 sambamba na miongozo ya kimataifa.

Kampuni ya Carbon Tanzania (CT Limited) imeingia ubia na jumuiya za uhifadhi wa wanyamapori (WMA) tano za Mkoa wa Ruvuma ambazo ni Jumuiya za Nalika na Chingoli katika Wilaya ya Tunduru na Jumuiya za Kisungule, Kimbanda na Mbarang`andu katika Wilaya ya Namtumbo.

Jumuiya hizo zina eneo lenye ukubwa hekta 856,600 ambazo ni sawa na kilometa za mraba 8,566 katika uanzishaji na utekelezaji wa mradi wa biashara ya hewa ukaa.

**Hatua Muhimu Katika Utekelezaji wa Mradi**

Novemba 2023, CT Limited ilitia saini mikataba na jumuiya za WMA kwa lengo la kuanzisha mradi wa biashara ya kaboni.

Ingawa mradi bado haujaanza kuuza vyeti vya kaboni, hatua za uhakiki na uthibitishaji zinaendelea, ambapo wataalamu kutoka NCMC wamekamilisha vipimo vya awali vya kaboni katika misitu ili kuhakikisha upatikanaji wa vyeti vya kuuza kaboni.

Ofisa mradi huo wa Kanda wa Ruvuma anasema hivi sasa, kampuni hiyo imewekeza zaidi ya shilingi bilioni 1.2 katika shughuli mbalimbali,na kwamba kati ya fedha hizo shilingi milioni 606 zimetumika katika kulinda maliasili na shilingi milioni 663 zimeelekezwa katika miradi ya maendeleo, huduma za jamii, elimu na ufuatiliaji wa mradi.

Anaitaja miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa miundombinu ya ofisi, madarasa, zahanati, nyumba za watumishi na madawati kwa shule na kwamba huduma za jamii pia zimeimarishwa kwa utoaji wa bima za afya na chakula shuleni.

> Kampuni hii inafanya shughuli za uhifadhi wa misitu ya asili kwa lengo la kufanya biashara ya kaboni kwa kuzingatia Kanuni za Biashara ya Kaboni za Tanzania, 2022 na marekebisho yake ya mwaka 2023 sambamba na miongozo ya kimataifa.

**Mpango wa Baadaye na Malengo ya 2025**

Katika mpango wake wa mwaka 2025, CT Limited imepanga kukamilisha maandiko ya mradi na kuyawasilisha kwa mamlaka husika na kufanikisha uthibitishaji wa mradi na kuuza vyeti vya kaboni ifikapo mwaka 2025/2026.


Mipango mingine ni kupanua mradi kwa kushirikiana na jumuiya mpya kama Ifinga na vijiji 12 vya Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvuma .

Mradi wa kaboni wa Ruvuma unatarajiwa kuwa mfano wa mafanikio kwa miradi mingine ya uhifadhi na maendeleo nchini Tanzania.



**BAADHI ya misitu ya asili inayopatikana mkoani Ruvuma.**

# Mafanikio bustani ya Ruhila




**MWONEKANO wa bustani ya Ruhila, Songea.**

## Bustani ya Ruhila Songea: Kivutio kinachochochea sekta ya utalii Ruvuma

**Na Albano Midelo**

Katika mkoa wa Ruvuma, bustani ya wanyamapori ya Ruhila iliyopo Manispaa ya Songea inajitokeza kama moja ya vivutio vinavyoendelea kuimarika kwa kasi, ikileta matumaini mapya kwa sekta ya utalii.

Pamoja na historia yake iliyoanzia kama Kikosi Dhidi ya Ujangili mwaka 1990, bustani hii sasa imekuwa eneo muhimu la burudani, uhifadhi wa wanyamapori, na chanzo cha mapato kwa serikali na jamii zinazozunguka.

### Mafanikio ya Bustani ya Ruhila

Bustani ya Ruhila imepiga hatua kubwa katika mapato na idadi ya wageni wanaotembelea eneo hilo. Kwa kipindi cha mwaka 2023/2024, bustani ilikusanya TZS 15,437,135, ikiwa imevuka shabaha ya TZS 10,208,000.

Hata hivyo, katika kipindi cha Julai-Septemba 2024, mapato yalipungua hadi TZS 5,167,640 dhidi ya lengo la TZS 7,622,000. Hali hii inaonyesha umuhimu wa mikakati endelevu ili kudumisha ongezeko la mapato.

### Mikakati ya Kukuza Utalii

Ili kuboresha utalii, mamlaka inayosimamia bustani hii imeweka mipango mbalimbali, ikiwa ni pamoja na:

- Kutangaza vivutio kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii.
- Kuboresha miundombinu ya utalii kama uzio na barabara.
- Kushirikiana na wadau wa sekta binafsi na umma katika uwekezaji.
- Kupeleka wanyamapori kwenye maonesho ya utalii.
- Kuhamasisha utalii wa ndani kwa kushirikisha shule, vyuo, na taasisi zingine.

Hifadhi ndogo ya asili ya wanyama ya Ruhila yenye ukubwa wa hekta 600 ilianzishwa mwaka 1974, ipo umbali wa kilometa saba kutoka mjini Songea.

### Miradi ya Maendeleo

Bustani ya Ruhila imewekeza kwenye miradi muhimu ili kuboresha huduma kwa watalii:

- **Campsite:** Jengo lililokamilika kwa Tsh 103,000,000 linalohudumia wageni kwa vinywaji na vyakula.
- **Mabanda ya Utalii:** Yaliyojengwa kwa Tsh 20,000,000 kwa madhumuni ya wageni kupumzika na kufurahia mandhari.
- **Vizuizi vya Wanyamapori:** Vyenye thamani ya Tsh 78,000,000, vikiwa na simba, tausi, kasuku, na ngedere.
- **Swimming Pool:** Imegharimu Tsh 62,529,984 na imekamilika kwa ubora wa hali ya juu.
- **Madaraja Madogo:** Yaliyojengwa kwa Tsh 101,000,000 ili kurahisisha utalii wa miguu na baiskeli.
- **Uzio wa Bustani:** Mradi unaoendelea wenye gharama ya Tsh 415,389,900, ukitarajiwa kukamilika Aprili 2025.

### Matarajio ya baadaye ya kuboresha bustani ya Ruhila

Ili kuhakikisha bustani ya Ruhila inaendelea kuwa kivutio kwa wageni mbalimbali mamlaka husika imependekeza

- Kuongeza idadi ya wanyamapori ili kuvutia wageni zaidi.
- Kutafuta fedha kwa ajili ya kampeni za kutangaza utalii wa ndani.
- Kuweka mikakati ya usafiri wa umma ili kurahisisha safari za wageni.
- Kuboresha barabara ya kutoka Msamala hadi bustani kwa kiwango cha lami.
- Kushirikiana na viongozi wa mkoa ili kuzuia uvamizi wa maeneo ya bustani

Hifadhi ndogo ya asili ya wanyama ya Ruhila yenye ukubwa wa hekta 600 ilianzishwa mwaka 1974,ipo umbali wa kilometa saba kutoka mjini Songea.

Afisa Utalii wa Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori (TAWA) katika hifadhi hiyo David Tesha amesema Bustani nyingi za wanyamapori zilizopo mjini zimetengenezwa na binadamu(Artificial Game Reserve),lakini bustani ya wanyamapori ya Luhira ni ya pekee ya asili nchini iliyopo mjini.

Kulingana na Afisa huyo wa TAWA bustani ya Luhira yote imewekewa uzio na kwamba ndani ya Hifadhi hiyo kuna aina mbalimbali za wanyama wakiwemo pundamilia,pofu,simba,nyumbu fisimaji, nyani,pongo tumbili, kakakuona,swalapala na kobe,pia bustani hiyo ni makazi ya reptilia na ndege wa aina mbalimbali.

Amesema Luhira zoo ni eneo la asili lenye utajiri wa miti ya miyom bo,misuku,mitumbitumbi,miwanga,minyonyo,mizambarau,minin ga, na mikuyu,na kwamba ni miongoni mwa bustani chache zenye uoto wa asili kabisa zilizopo mjini.



**BAADHI ya miundombinu iliyojengwa na inayoendelea kujengwa ndani ya bustani ya Ruhila.**




**BAADHI ya wanyama wanaopatikana ndani ya bustani ya Ruhila.**

# Mazingira yenye uhai: Safari ya shamba la miti Wino katika uhifadhi na maendeleo

**Na ALBANO MIDELO**

Katika mkoa wa Ruvuma, ndani ya mandhari tulivu Halmashauri ya Madaba wilayani Songea, lipo shamba la miti la Wino, mojawapo ya mashamba 24 yanayosimamiwa na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS).

Mhifadhi Mkuu wa shamba hilo Glory Kasmiri anasema shamba likiwa na ukubwa wa hekta 39,718, limekuwa na mchango mkubwa katika uhifadhi wa mazingira, utoaji wa ajira, na maendeleo ya jamii inayolizunguka.

**Historia ya Shamba la Wino**

Shamba hili lilianzishwa mwaka 2010 kwa kuanzia na hekta 2,259 za msitu wa asili katika eneo la Wino. Baadaye, mwaka 2014 na 2016, vijiji vya Mkongotema na Ifinga vilitoa maeneo zaidi na hivyo kuongeza ukubwa wa shamba hadi kufikia hali ya sasa. Tangu kuanzishwa kwake, zaidi ya hekta 5,495 zimepandwa miti ya aina mbalimbali, hasa miti ya misindano.

**Mchango kwa Jamii**

Mbali na jukumu lake la msingi la uhifadhi wa mazingira, shamba la Wino limekuwa mshirika muhimu wa maendeleo katika jamii inayolizunguka.

Katika kipindi cha miaka minne (2018-2022), shamba hili limechangia zaidi ya shilingi milioni 514 kwa miradi ya kijamii. Mchango huu umesaidia katika ujenzi wa shule, makanisa na miradi ya maji, ikiwa ni pamoja na mradi wa maji wa Kijiji cha Ifinga uliogharimu shilingi milioni 482.

Miongoni mwa misaada iliyotolewa ni:

- Mifuko 100 ya saruji kwa shule ya msingi Turiani na Lilondo (shilingi 1,450,000).
- Mabati 100 kwa shule ya sekondari Wino (shilingi 2,450,000).
- Mizinga ya nyuki 30 kwa kijiji cha Igawisenga (shilingi 3,000,000).
- Madirisha ya aluminium 9 kwa kijiji cha Mkongotema (shilingi 2,489,800).

Shughuli za upandaji miti zimeendelea kwa kasi, ambapo takwimu zinaonesha kuwa kati ya mwaka 2010 na 2022, miche 6,634,119 ilikuzwa, na kati ya hiyo, miche 6,157,947 ilipandwa. Kwa mwaka 2022 pekee, miche 717,119 ilikuzwa, huku 565,499 ikipandwa.



MENEJA wa shamba la miti Wino Mhifadhi Glory Kasmiri akielekeza jambo.

**Upandaji wa Miti na Uhifadhi wa Mazingira**

Shughuli za upandaji miti zimeendelea kwa kasi, ambapo takwimu zinaonesha kuwa kati ya mwaka 2010 na 2022, miche 6,634,119 ilikuzwa, na kati ya hiyo, miche 6,157,947 ilipandwa. Kwa mwaka 2022 pekee, miche 717,119 ilikuzwa, huku 565,499 ikipandwa.

**Ajira na Mustakabali wa Shamba la Wino**

Shamba hili limekuwa chanzo kikubwa cha ajira, likitoa nafasi za kazi kwa wafanyakazi wa kudumu 15, wafanyakazi wa mikataba 10, na vibarua wa msimu wapatao 4,000 kwa mwaka.

Kwa malengo ya muda mrefu, ifikapo mwaka 2025, shamba linapanga kupanua upandaji wa miti kufikia hekta 3,000 kwa mwaka, kuimarisha miundombinu, na kushirikiana na jamii katika utunzaji wa mazingira.

Kwa mafanikio haya, shamba la miti Wino linaendelea kuwa mfano wa jinsi uhifadhi wa mazingira unavyoweza kwenda sambamba na maendeleo ya kijamii na kiuchumi.



MWONEKANO wa shamba la miti la Wino Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma.




# MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

## MAFANIKIO MANISPAA YA SONGEA



MWONEKANO wa sekondari mpya ya Dkt. Lawrence Gama iliyojengwa Manispaa ya Songea kupitia pragramu ya SEQUIP



MKURUGENZI wa Manispaa ya Songea Wakili Bashiri Muhoja



MKUU wa Wilaya ya Songea Mheshimiwa Kapenjama Ndile



MSTAHIKI Meya wa Manispaa ya Songea Michael Mbano

**WASILIANA NASI**

SONGEA MUNICIPAL COUNCIL
**Anuani ya Posta:** P O BOX 14, SONGEA
**Simu ya Mezani:** 025 2602970
**Simu ya Kiganjani:**
**Barua Pepe:** info@songeamc.go.tz

***MAFANIKIO YA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS SAMIA MANISPAA YA SONGEA***

# MAFANIKIO YA MIRADI YA MAENDELEO KATIKA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS SAMIA MANISPAA YA SONGEA

**Na ALBANO MIDELO**

Katika kipindi cha miaka minne ya uongozi wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. Samia Suluhu Hassan, miradi mbalimbali ya maendeleo imefanikiwa kutekelezwa katika sekta tofauti ndani ya Manispaa ya Songea mkoani Ruvuma.

Mkurugenzi wa Manispaa ya Songea Wakili Bashir Muhoja anasema Miradi hii imelenga kuboresha huduma za jamii, kukuza uchumi wa eneo husika, na kuimarisha ustawi wa wananchi kwa ujumla.

**Muhtasari wa Miradi Kisekta**

Miradi iliyotekelezwa inajumuisha sekta muhimu kama afya, elimu, miundombinu, kilimo, na maendeleo ya jamii. Hii hapa ni orodha ya baadhi ya sekta na thamani ya miradi iliyotekelezwa:

- **Afya**: Miradi yenye thamani ya TZS 14.6 bilioni imetekelezwa, ikiwa ni pamoja na ujenzi wa vituo vya afya na ununuzi wa vifaa tiba.
- **Elimu**: Sekta ya elimu (msingi na sekondari) imepokea miradi yenye thamani ya TZS 22.8 bilioni, ikihusisha ujenzi wa madarasa, mabweni, na ununuzi wa vifaa vya kufundishia.
- **Miundombinu**: Miradi mikubwa ya ujenzi wa barabara na miundombinu mingine ina thamani ya TZS 44.9 bilioni, ikilenga kuboresha usafiri na uchukuzi.
- **Kilimo na Mifugo**: Sekta hii imepata miradi yenye thamani ya TZS 1.46 bilioni, ikiwa ni pamoja na uimarishaji wa huduma za ugani na masoko ya mazao.
- **Maendeleo ya Jamii**: Miradi ya maendeleo ya jamii yenye thamani ya TZS 2.37 bilioni imetekelezwa kwa lengo la kuinua maisha ya wananchi na kuimarisha ustawi wa jamii.
- **Ujenzi na Miundombinu**: Jumla ya TZS 3.22 bilioni zimetumika katika miradi ya ujenzi na ukarabati wa majengo ya serikali na miundombinu mingine muhimu.
- **Utawala**: Miradi yenye thamani ya TZS 3.03 bilioni imetekelezwa ili kuboresha mazingira ya utendaji wa serikali za mitaa.



MWONEKANO wa Shule ya Msingi Chifu Zulu iliyojengwa na serikali kupitia Programu ya BOOST Kata ya Mshangano Manispaa ya Songea, shule hiyo inachukua wanafunzi wa shule ya msingi na ilizunduliwa Septemba 2024 na Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan.

Katika kipindi hiki cha miaka minne, serikali imetekeleza miradi ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya **TZS 276.05 bilioni**, ambapo **TZS 251.15 bilioni** zilipokelewa na kutumika katika utekelezaji.

**Jumla ya Fedha Zilizotumika**

Katika kipindi hiki cha miaka minne, serikali imetekeleza miradi ya maendeleo yenye jumla ya thamani ya **TZS 276.05 bilioni**, ambapo **TZS 251.15 bilioni** zilipokelewa na kutumika katika utekelezaji.

Serikali ya Awamu ya Sita chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan imeonyesha dhamira ya dhati ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Songea kupitia miradi mbalimbali ya maendeleo. Kupitia uwekezaji huu, wananchi wameweza kupata huduma bora zaidi za afya, elimu, miundombinu, na sekta nyingine muhimu. Kwa mafanikio haya, ni wazi kuwa juhudi za kuimarisha ustawi wa jamii zinaendelea, na matarajio ya maendeleo zaidi yanabaki kuwa ya kuahidi kwa siku zijazo.



MWONEKANO wa Mji wa Songea



MWONEKANO wa majengo ya Hospitali ya Manispaa ya Songea iliyojengwa eneo la Sanangula. Hospitali hiyo imeanza kutoa huduma za msingi kwa wananchi.




# MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA

## MAFANIKIO MBINGA MJI



**JENGO la Halmashauri ya Mji wa Mbinga**



MKURUGENZI Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Amina Khamis Sefu



MKUU wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisare Makori



MWENYEKITI wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Mheshimiwa Kelvin Mapunda

**WASILIANA NASI**
Sanduku la Barua: P.O.BOX 135 ;
Simu ya Mezani: +225 - 2640664 ;
Mobile: 0733216557 ;
Barua pepe: td@mbingatc.go.tz

## *MAFANIKIO YA UTEKELEZAJI WA MIRADI MBINGA MJI CHINI YA RAIS SAMIA*



MRADI wa shule mpya ya sekondari Kata ya Matarawe mjini Mbinga, ambayo imejengwa kupitia Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari SEQUIP (Development Journalist).

**Na ALBANO MIDELO**

HALMASHAURI ya Mji wa Mbinga mkoani Ruvuma imepiga hatua kubwa katika maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kupitia utekelezaji wa miradi mbalimbali chini ya uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mji wa Mbinga Amina Khamis Sefu anasema miradi hii imehusisha sekta ya elimu, miundombinu na huduma za jamii, ikichochea ustawi wa wananchi na kuboresha maisha yao kwa ujumla.

**Maendeleo Katika Sekta Mbalimbali**

**1. Sekta ya Elimu**

Katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, serikali imewekeza kiasi kikubwa cha fedha katika sekta ya elimu. Baadhi ya miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

- **Ujenzi wa shule mpya Lusonga** – 470,000,000 TZS (Mradi unatumika).
- **Ujenzi wa shule mpya Dr. Philip I. Mpango Sekondari** – 560,552,287 TZS (Inatumika).
- **Ujenzi wa matundu ya vyoo 6 Luhuwiko Sekondari** – 6,600,000 TZS (Yanatumika).
- **Umaliziaji wa maabara moja Kindimba Sekondari** – 30,000,000 TZS (Imekamilika).
- **Umaliziaji wa vyumba vya madarasa 4 Kindimba** – 50,000,000 TZS (Yamekamilika na yanatumika).

**2. Sekta ya Miundombinu**

Serikali pia imewekeza katika ujenzi wa miundombinu muhimu kama barabara, huduma za afya, na maji safi kwa wananchi. Hii imesaidia kupunguza changamoto za usafiri na upatikanaji wa huduma za msingi.

**3. Huduma za Jamii**

Miradi ya kuboresha huduma za afya, upatikanaji wa maji, na miradi mingine ya kijamii imeendelea kutekelezwa kwa mafanikio makubwa, hivyo kuinua hali ya maisha ya wananchi wa Mbinga.


**Fedha Zilizotumika**

Jumla ya **12,121,869,723 TZS** zimetumika katika utekelezaji wa miradi hii katika kipindi cha miaka mitatu.

Uwekezaji huu mkubwa katika miundombinu na huduma za jamii umeleta mafanikio makubwa kwa wananchi wa Mbinga Mji. Serikali inaendelea kuhakikisha kuwa miradi inayotekelezwa inaleta matokeo chanya na kuchangia katika maendeleo ya taifa kwa ujumla. Kwa juhudi hizi, maisha ya wananchi yanazidi kuboreka na mustakabali wa maendeleo unaonekana kuwa mzuri.

**MAFANIKIO**

Serikali pia imewekeza katika ujenzi wa miundombinu muhimu kama barabara, huduma za afya na maji safi kwa wananchi. Hii imesaidia kupunguza changamoto za usafiri na upatikanaji wa huduma za msingi.




# MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA
# MAFANIKIO MBINGA




Jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ambalo lilifunguliwa rasmi na Rais Dkt.Samia Suluhu Hassan



Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura



Mkuu wa Wilaya ya Mbinga Mheshimiwa Kisare Makori



Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Deusderius Haule

**WASILINA NASI**
MBINGA DISTRICT COUNCIL
**Sanduku la posta:** P.O. BOX 194
MBINGA-RUVUMA
**Namba za simu:** 2552640005
**Simu ya mkononi:** PS 0754533018
**parua pepe:** ded@mbingadc.go.tz

## MIRADI YA MBINGA INAVYOGUSA MAISHA YA WANANCHI

# MIRADI YA MBINGA INAVYOGUSA MAISHA YA WANANCHI



Baadhi ya majengo katika mradi wa ujenzi hospitali mpya ya Halmashauri ya MbInga ambayo imeanza kuhudumia wananchi

**Na ALBANO MIDELO**

Katika jitihada za kuboresha huduma za kijamii na kuimarisha ustawi wa wananchi, Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga mkoani Ruvuma imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025. Miradi hii imegawanyika katika sekta kadhaa ikiwemo afya, elimu, miundombinu, kilimo na uwezeshaji wa wananchi kiuchumi

**1. Sekta ya Afya**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga Joseph Kashushura anasema miradi ya afya imejikita katika ujenzi wa vituo vya afya, hospitali na zahanati pamoja na ukamilishaji wa majengo ya OPD na maabara.

Anasema ukamilishaji wa wodi tatu katika Hospitali ya Wilaya umetekelezwa kwa kutumia shilingi milioni 95. Aidha, ujenzi wa jengo la upasuaji katika hospitali hiyo unaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 350.

**2. Sekta ya Elimu**

Katika sekta ya elimu, halmashauri imejikita katika ujenzi na ukarabati wa madarasa, ofisi za walimu, nyumba za walimu na matundu ya vyoo. Miongoni mwa miradi inayotekelezwa ni ujenzi wa madarasa 2 katika Shule ya Msingi Njombe kwa gharama ya shilingi milioni 10 na ukamilishaji wa hosteli ya wanafunzi katika Sekondari ya Mikalanga kwa shilingi milioni 30.

**3. Miundombinu ya Jamii**

Halmashauri pia imewekeza katika ujenzi wa ofisi za kata na vijiji, jengo la uwekezaji mjini Mbinga pamoja na kiwanja cha michezo. Kukarabati jengo la uwekezaji kwa gharama ya sh. milioni 570, huku ujenzi wa jengo la uwezeshaji wananchi kiuchumi ukiwa mbioni kuanza.

**4. Kilimo na Uwezeshaji Wananchi**

Katika jitihada za kuinua sekta ya kilimo, halmashauri imeanzisha shamba la kuzalisha miche ya kahawa lenye ukubwa wa hekta 33 kwa sh.milioni 50.

Aidha, mpango wa kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa vijana, wanawake na watu wenye ulemavu umefadhiliwa kwa sh. milioni 739.5, lakini fedha hizo bado hazijatolewa kwa walengwa.

**Jumla ya fedha zilizotumika**

Kwa mwaka wa fedha 2024/2025, jumla ya sh. bilioni 6.18 zilitengewa miradi mbalimbali. Hadi sasa, sh. bilioni 3.40 zimepokelewa, huku sh. bilioni 1.24 zikiwa zimetumika kwenye utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga imeonyesha dhamira ya dhati ya kuimarisha maendeleo ya wananchi wake kupitia miradi mbalimbali inayotekelezwa. Hata hivyo, changamoto ya upatikanaji wa fedha kwa wakati inakwamisha utekelezaji wa baadhi ya miradi. Ni matumaini ya wananchi kuwa miradi itakamilika kwa wakati na kuleta manufaa yaliyokusudiwa kwa jamii.

**MILIONI 95**

*Imetumika kwenye ukamilishaji wa wodi tatu Hospital ya Wilaya. Aidha, ujenzi wa jengo la upasuaji katika hospitali hiyo unaendelea kwa gharama ya shilingi milioni 350.*






# MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA
## MAFANIKIO NYASA



**JENGO la Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa**



**MKURUGENZI wa Halmashauri ya Nyasa Khalid Khalif**



**MKUU wa Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Pers Magiri**



**MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Mheshimiwa Starwat Nombo**

**CONTACT US**

Nyasa District Council
**Postal Address:** Box 90 Mbamba bay
**Telephone:** 025 -2952003
**Mobile:**
**Email:** ps.ded@nyasadc.go.tz

## *RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA HUDUMA ZA JAMII NYASA*

# RAIS SAMIA ALIVYOBORESHA HUDUMA ZA JAMII NYASA

Sekta ya afya imepokea jumla ya shilingi 2,240,878,950 za ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu muhimu katika maeneo mbalimbali

**Na ALBANO MIDELO**

Katika jitihada za kuboresha huduma za kijamii, Wilaya ya Nyasa iliyopo katika Mkoa wa Ruvuma imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kati ya mwaka wa fedha 2021 hadi 2025, kwa jumla ya shilingi 5,898,886,215.11.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Nyasa Khalid Khalif anasema miradi hiyo imegusa sekta mbalimbali muhimu zikiwemo afya, elimu na utawala.

**Miradi ya Afya**

Sekta ya afya imepokea jumla ya shilingi 2,240,878,950 za ujenzi na ukamilishaji wa miundombinu muhimu. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni:

- Ujenzi wa jengo la upasuaji na wodi ya kina mama katika Kituo cha Afya Liparamba (Tsh 250,000,000).
- Ujenzi wa OPD na maabara (Tsh 250,000,000).
- Ujenzi wa nyumba za watumishi wa afya (Tsh 90,000,000).
- Ujenzi wa jengo la dharura EMD katika Hospitali ya Wilaya (Tsh 300,000,000).
- Uendelezaji wa ujenzi wa Kituo cha Afya Kingerikiti (Tsh 300,000,000).
- Ujenzi wa zahanati katika maeneo ya Jangwani, Lundu, na Chimate (Tsh 50,000,000 kila moja).
- Uendelezaji wa Hospitali ya Wilaya (Tsh 800,000,000).

**Miradi ya Elimu**

Sekta ya elimu imepatiwa kiasi cha shilingi 2,101,218,265.11 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, maabara, na miundombinu ya shule. Miradi muhimu ni pamoja na:

- Ujenzi wa vyumba 44 vya madarasa katika shule za sekondari 16 (Tsh 880,000,000).
- Ujenzi wa shule mpya ya Sekondari ya Kata ya Liwundi (Tsh 470,000,000).
- Ujenzi wa vyumba 10 vya madarasa katika vituo shikizi vya shule za msingi (Tsh 200,000,000).
- Ujenzi wa vyumba vya maabara za sayansi katika shule mbalimbali za sekondari (Tsh 150,000,000).
- Ujenzi na ukamilishaji wa matundu ya vyoo katika shule mbalimbali (Tsh 180,000,000).

**Miradi ya Utawala**

Kwa upande wa sekta ya utawala, kiasi cha shilingi 1,488,028,000 kimetumika kutekeleza miradi ifuatayo:

- Ujenzi wa nyumba za wakuu wa idara (Tsh 150,000,000).
- Uendelezaji wa ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya (Tsh 1,338,028,000).

**Jumla ya Fedha Zilizotumika**

Kwa mujibu wa takwimu za utekelezaji wa miradi hii, jumla ya fedha zilizotumika ni shilingi 5,898,886,215.11. Miradi mingi imeshakamilika na inatumika, huku baadhi ikiwa katika hatua za mwisho za ukamilishaji.

Utekelezaji wa miradi hii umeleta maboresho makubwa katika huduma za afya, elimu, na utawala ndani ya Wilaya ya Nyasa. Wananchi sasa wanapata huduma bora na za uhakika, huku miundombinu ikiimarika kwa kiwango kikubwa.



MRADI wa Shule mpya ya Sekondari Kata ya Riwundi iliyojengwa kupitia Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari SEUIP





MWONEKANO wa majengo ya Hospitali ya Wilaya ya Nyasa ambayo ujenzi wake umekamilika na hospitali hiyo inatoa huduma kwa wananchi.




# MIAKA MINNE YA RAIS DK. SAMIA
# MAFANIKIO TUNDURU


UJENZI wa Sekondari Kata ya Tuwemacho Tunduru ambayo imekamilika na kuanza kuchukua wanafunzi.


MKURUGENZI wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando


MKUU wa Wilaya ya Tunduru Mheshimiwa Simon Chacha


MWENYEKITI wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Mheshimiwa Hairu Hemed Musa

**WASILIANA NASI**

Halmashauri ya Wilaya Tunduru
**Anuani ya Posta:** 275, TUNDURU
**Simu:** + 255-025-2680004
**Simu ya Nununu:**
**Barua Pepe:** info@tundurudc.go.tz

## *TUNDURU INAVYOJIVUNIA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS SAMIA*



BAADHI ya mabweni mapya yaliyojjengwa na serikali katika Shule ya Sekondari ya Masonya P.o Box 600 Songea, Ruvuma - Tanzania.



MRADI wa ukarabati wa hospitali kongwe ya Tunduru.

# TUNDURU INAVYOJIVUNIA MIAKA MINNE YA UONGOZI WA RAIS SAMIA

**Na ALBANO MIDELO**

Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru mkoani Ruvum, imekuwa mstari wa mbele katika kuhakikisha miradi mbalimbali ya maendeleo inatekelezwa kwa manufaa ya wananchi. Kuanzia mwaka wa fedha 2020/21 hadi Januari 2025, jumla ya miradi mingi imekamilishwa au inaendelea kutekelezwa, ikihusisha sekta za elimu, afya, miundombinu, maji, na maendeleo ya kijamii.

**Miradi ya Elimu**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru Chiza Marando anasema Halmashauri hiyo imewekeza pakubwa katika uboreshaji wa miundombinu ya elimu. Ujenzi wa madarasa, mabweni, vyoo na maabara umekuwa kipaumbele ili kuhakikisha wanafunzi wanapata mazingira bora ya kusomea.

Kwa mwaka 2021/22 pekee, zaidi ya shilingi bilioni 8.2 zilitumika katika miradi mbalimbali ya elimu, ikiwemo ujenzi wa shule mpya na ukarabati wa shule kongwe.

Katika mwaka wa fedha 2022/23, halmashauri ilitumia zaidi ya shilingi bilioni 6.7 za ujenzi wa madarasa, mabweni, matundu ya vyoo, na kuboresha miundombinu ya shule za msingi na sekondari. Mwaka 2023/24 uliendelea na kasi hiyo, ambapo zaidi ya shilingi bilioni 6.7 zilitengwa kwa uboreshaji wa elimu, huku mwaka 2024/25 ukishuhudia matumizi ya zaidi ya shilingi bilioni 2.9 kufikia Januari, 2025.

**Sekta ya Afya**

Maendeleo ya huduma za afya pia yamepewa kipaumbele kwa miaka hii mitano. Ukarabati wa hospitali ya wilaya ya Tunduru, ujenzi wa vituo vya afya, zahanati na ununuzi wa vifaa tiba umekuwa sehemu muhimu ya matumizi ya bajeti ya halmashauri. Miongoni mwa miradi iliyotekelezwa ni ujenzi wa vituo vya afya vya Masonya, Mchesi, Nalasi, na Nampungu, pamoja na ukamilishaji wa wodi mbili katika Hospitali ya Wilaya ya Tunduru.

> Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa miradi (2020/21 - 2024/25), jumla ya shilingi 24,683,926,557.09 zilitumika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Tunduru.

**Miundombinu na Huduma za Jamii**

Halmashauri pia imejikita katika ujenzi wa barabara, uchimbaji wa visima vya maji, ujenzi wa vyoo vya umma, na miradi ya nishati. Maeneo ya vijijini yamepewa kipaumbele ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za kijamii.

**Jumla ya Fedha Zilizotumika**

Katika kipindi cha miaka mitano ya utekelezaji wa miradi (2020/21 - 2024/25), jumla ya shilingi **24,683,926,557.09** zilitumika kufanikisha miradi mbalimbali ya maendeleo katika Wilaya ya Tunduru.

Tunduru DC inajivunia hatua hizi kubwa za maendeleo na inaendelea kushirikiana na serikali kuu, wadau wa maendeleo na wananchi ili kuhakikisha malengo ya maendeleo yanafikiwa kwa manufaa ya wote.



MRADI wa kituo cha afya Kata ya Masonya wilayani Tunduru ambacho kimeanza kutoa huduma kwa wananchi.



BAADHI ya majengo ya madarasa ambayo yamejengwa katika sekondari ya wasichana Masonya Tunduru.

# MADABA YAJIVUNIA MAFANIKIO MAKUBWA YA MAENDELEO

**Na ALBANO MIDELO**

Katika kipindi cha miaka minne iliyopita, Halmashauri ya Madaba Wilaya ya Songea mkoani Ruvuma, imepiga hatua kubwa katika sekta mbalimbali za maendeleo. Kwa kuungwa mkono na Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, miradi yenye thamani ya zaidi ya shilingi bilioni 19 imefanikiwa kutekelezwa, ikihusisha sekta za elimu, afya, kilimo na utawala.

**Elimu: Miundombinu Bora kwa Wanafunzi**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Madaba Sajidu Idrisa Mohamed anasema katika sekta ya elimu, zaidi ya shilingi bilioni 8.18 zimetumika kuboresha mazingira ya kujifunzia kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari.

Kwa kipindi cha mwaka 2020 hadi 2025, Madaba imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 121, matundu ya vyoo 286, shule mpya tano, maabara 14, hosteli tano na nyumba za walimu 13. Mafanikio haya yamechangia ongezeko la ufaulu na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

**Afya: Huduma za Kisasa kwa Wananchi**

Katika kuhakikisha wananchi wanapata huduma bora za afya, serikali imetumia zaidi ya shilingi bilioni 4.3 kuboresha sekta hiyo. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Madaba umekamilika, ukiwa na majengo yote muhimu, zikiwemo maabara, wodi za wagonjwa, jengo la mama na mtoto na chumba cha upasuaji. Pia, zahanati tano na kituo cha afya kimoja vimejengwa, huku magari manne ya afya yakinunuliwa kusaidia huduma za dharura.

> Kwa kipindi cha 2020 hadi 2025, Madaba imefanikiwa kujenga vyumba vya madarasa 121, matundu ya vyoo 286, shule mpya tano, maabara 14, hosteli tano, pamoja na nyumba za walimu 13. Mafanikio haya yamechangia ongezeko la ufaulu na kupunguza msongamano wa wanafunzi darasani.

**Kilimo: Uhakika wa Chakula na Masoko**

Kilimo kikiwa uti wa mgongo wa uchumi wa Madaba, zaidi ya shilingi bilioni 4.5 zimetolewa kwa ujenzi wa maghala tisa ya kuhifadhi mazao, pikipiki 22 kwa maofisa ugani, pamoja na mashine ya kisasa ya kupima udongo. Hatua hii imeongeza uzalishaji wa mazao kutoka tani 41,716 mwaka 2021 hadi tani 160,343 mwaka 2024, huku upatikanaji wa mbolea ya ruzuku ukifikia asilimia 97.7 ya mahitaji.

**Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi**

Katika kuinua uchumi wa wananchi, zaidi ya shilingi milioni 160 zimetolewa kama mikopo isiyo na riba kwa vikundi vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Hili ni ongezeko la asilimia 232 kutoka milioni 48 zilizotolewa mwaka 2020. Aidha, soko la kisasa lenye thamani ya shilingi milioni 190 limejengwa katika Kijiji cha Lituta, likiwa na vizimba 84 na vyoo vya kisasa.

**Utawala: Mazingira Bora kwa Watumishi**

Kwa upande wa utawala, shilingi bilioni 1.25 zimetumika kujenga ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, nyumba tano za wakuu wa idara, pamoja na ununuzi wa magari matatu kwa ajili ya usimamizi wa miradi na huduma kwa wananchi.

Serikali ya Awamu ya Sita imeendelea kuonesha dhamira yake ya dhati ya kuwaletea wananchi wa Madaba maendeleo yanayogusa maisha yao moja kwa moja. Wananchi sasa wana matumaini makubwa ya siku za usoni, wakiendelea kufurahia matunda ya uwekezaji mkubwa wa serikali katika kila sekta muhimu.



SHULE ya Sekondari mpya Kata ya Lilondo Halmashauri ya Madaba wilayani Songea iliyojengwa na serikali kupitia Programu ya Uboreshaji Elimu ya Sekondari Nchini (SEQUIP) imekamilika na kuanza kuchukua wanafunzi



MWONEKANO wa majengo katika Hospitali ya Halmashauri ya Madaba.

# MAFANIKIO YA SERIKALI YA AWAMU YA SITA WILAYANI NAMTUMBO (2020-2023)

**TSh 38,586,195,318.24.**
Fedha hizi zimetumika katika sekta tofauti zinazolenga kuboresha huduma za jamii na kukuza ustawi wa wananchi.



WANAFUNZI wa sekondari hiyo yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi wa kike kuanzia kidato cha kwanza hadi cha sita

**Na ALBANO MIDELO**

Katika kipindi cha uongozi wa Serikali ya Awamu ya Sita chini ya Rais Dkt. Samia Suluhu Hassan, Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma imefanikiwa kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa gharama ya jumla ya **TSh 38,586,195,318.24**.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Namtumbo Philemon Magesa anasema fedha hizo zimetumika katika sekta tofauti zinazolenga kuboresha huduma za jamii na kukuza ustawi wa wananchi.

**Muhtasari wa Miradi Kisekta**

**1. Sekta ya Elimu**

Serikali imewekeza kwa kiasi kikubwa katika kuboresha miundombinu ya elimu kwa kujenga na kukamilisha:

- Vyumba vya madarasa katika shule za msingi na sekondari.
- Maktaba na maabara za shule za sekondari.
- Mabweni kwa wanafunzi wa shule za sekondari.
- Vifaa vya kufundishia na kujifunzia.

**2. Sekta ya Afya**

Kupitia mpango wa kuboresha huduma za afya, miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

- Ujenzi wa hospitali ya wilaya na vituo vya afya.
- Ujenzi wa zahanati katika vijiji mbalimbali.
- Ununuzi wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi.
- Uboreshaji wa huduma za lishe kwa watoto chini ya miaka mitano.

**3. Sekta ya Maji**

Serikali imeboresha huduma za maji kwa:

- Ujenzi wa miundombinu ya maji safi na salama.
- Ukarabati wa visima na mabwawa ya maji.
- Uboreshaji wa mifumo ya usambazaji wa maji vijijini.

**4. Sekta ya Maendeleo ya Jamii**

Katika kukuza maendeleo ya jamii na kuinua maisha ya wananchi, serikali imetekeleza:

- Utoaji wa mikopo kwa vikundi vya wanawake, vijana, na watu wenye ulemavu.
- Uimarishaji wa ruzuku kwa kaya masikini kupitia mfuko wa TASAF.
- Kampeni za uhamasishaji wa usawa wa kijinsia na haki za watoto.

Mafanikio haya yanaonesha dhamira ya Serikali ya Awamu ya Sita katika kuhakikisha ustawi wa wananchi wa Namtumbo unaboreshwa kupitia uwekezaji wa miradi ya maendeleo. Wananchi wa Namtumbo wanaendelea kushuhudia mabadiliko makubwa katika huduma za msingi kama elimu, afya, na maji, hali inayochochea ukuaji wa kijamii na kiuchumi.

Hii ni ishara kwamba serikali inaendelea kutekeleza ahadi zake kwa vitendo, huku ikihamasisha ushirikiano wa sekta binafsi na jamii kwa ujumla katika kuleta maendeleo endelevu.



MWONEKANO wa majengo katika Hospitali ya Wilaya ya Namtumbo mkoani Ruvuma.

UHURU
KIJANI
Alhamisi Aprili 3, 2025





JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MKUU WA MKOA RUVUMA

# ASANTENI WASHIRIKA

*Bodi ya Wakurugenzi, Menejimenti na Wafanyakazi wa Uhuru Publications Ltd, inawashukuru na kuwapongeza kwa kufanikisha uandaaji wa toleo maalumu la mafanikio ya Mkoa wa Ruvuma.*

KWA MAKALA, MATANGAZO YA BIASHARA WASILIANA NASI KWA SIMU NAMBA 0765-142-207 AU 0683-378-522



Gazeti hili hutolewa na Uhuru Publications Limited, S.L.P. 9221 Dar es Salaam